

HUYU MELKIZEDEKI NI NANI?



Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi.

Baba mpendwa uliye mbiguni, tunaposikia wimbo huu wa Amini Tu; inatufanya tujue ya kwamba hiyo tu ndiyo itupasayo kufanya kurithi yo yote ya ahadi za Mungu, kuziamini tu. Kwa kuwa imeandikwa, “Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.” Tunapolia kama yule mtu aliyekuwa na mtoto mwenye kifafa, “Bwana, naamini, nisaidie kutokuamini kwangu!” . . .

² Tunakushukuru kwa uweza wako mkuu, kule kujifunua Kwako kuu kwa ajili yetu katika siku hizi za mwisho. Inaifanya mioyo yetu iwe na furaha na shangwe kujua ya kwamba tumeunganishwa na Mungu aliye Hai. Ambaye hujithibitisha katika mwili, ushahidi wa vitu, kama alivyofanya siku zilizopita na kama alivyoahidi kwa ajili ya siku hizi. Tunashukurani nyingi sana Kwako Mungu wetu. Katika siku hizi zenye giza ambapo yaonekana hamna mtu anayejua ataiendea njia ipi, tunashukuru sana ya kwamba tulipata mahali salama, kimbilio.

³ Naam, tubariki usiku wa leo, Bwana, tunaponena Neno Lako. Na ahadi ambazo tumepewa, na tuzitunze mioyoni mwetu, tukazilinde kwa kicho, na tukazizingatie kwa nidhamu halisi ya uungu. Kwa kuwa tunaomba katika jina la Yesu, Amina.

⁴ Matoleo ya upendo? Haikuwapasa kufanya hivyo. Nani aliyefanya hivyo? Unahatia? Nilikuwa nikimkemea msimamizi. Anasema eti alichukua matoleo ya upendo kwa ajili yangu. Haikumpasa kufanya hivyo. Naifurahia, Mungu anajua hivyo; bali si—sikuja kwa ajili hiyo. Asanteni. Mungu na awabariki! Nitafanya kila kitu niwezacho. . . Nitaiweka moja kwa moja kwenye umishemari wa nchi za ng’ambo, ndivyo nitakavyojua ya kwamba itatumiwa kwa ufalme wa Mungu. Na Mungu akipenda, nitaichukua mwenyewe kwenda ng’ambo kuleta Injili ile ile ambayo mmekua mkiketi, mkiisikiza juma hili. Ndipo nitajua itatendwa kama mlivyoamini. Mungu na anisaidie kufanya hivyo.

⁵ Ninafuraha sana kwa sababu ya kuhudhuria kukubwa juma hili, na kwenu nyote watu ambao mnasikiza kwa simu usiku huu tena kwa—waya za simu. Nasi tuna furaha kwa kila mmoja wenu.

⁶ Billy aliniambia asubuhi ya leo, akasema, “Baba, kama ungalikuja nami asubuhi ya leo, alfajiri, baada tu ya mapambazuko, na kusimama nje mahali hapa na kuona kina mama wakiwalisha watoto wao motokaani, maskini watu hao wakiketi katika mvua wakingojea milango ifunguliwe. . .” Mnaona ningalikuwa mnafiki jinsi gani kama ningaliwaambieni

kinginecho ila ukweli? Ningalikuwa bila shaka mtu mbaya. Wakati mwingine sina budi kuumiza, bali si kwa kuwa nataka kufanya hivyo, ni kwa sababu... Si—si mimi ninayeumiza, ni ukweli unaoumiza. Nami ni—ni... Bali naamini hiyo ndiyo sababu yenu kuja. Kwa sababu mimi ni mwaminifu sana kwenu na ninafanya yote niwezayo kuwasaidia. Mungu na amsaidieni kila mmoja wenu.

⁷ Na sasa, nataka kuwashukuru watu kwa ushirikiano wao mzuri, wenyeji wa mji huu pia, waliotupa—wakaturuhusu hili—kukodisha jumba hili la shule, jumba la mikutano, pamoja na jumba hili la michezo. Nami nataka kuwashukuru wale maafisa kama mko hapa. Na pia nataka kumshukuru Thurston Colvin, ambaye ni msimamizi hapa, kwa ushirikiano wake mwema katika kutusaidia kupata hili na kuwa pamoja nasi kila usiku.

⁸ Tunashukuru idara ya polisi ya Jeffersonville kwa kuja huku na kulinda kwa gharama nafuu sana. Nafikiri wanalipwa dola mbili kwa saa ili polisi kuwa humu kwa jukumu maalum la kuweka motokaa kiwanjani, na kuona kwamba hamna—hamtendeki jambo lo lote, na kila kitu ni shwari. Tunawashukuru watu kwa ajili hiyo. Na kwa yule—yule—pia fundi wa mitambo kwenye—ubaoni, nilimwona. Na wote wanaoshirikiana nasi, tunawashukuru sana.

⁹ Nawashukuru kila mmoja wenu kwa zile zawadi. Billy ameniletea tu adhuhuri ya leo za—zawadi, zawadi nyingi katika vijisanduku, peremende na vinginevyo. Na moja yazo ilikuwa zile—zile safu za Heri pamoja na picha ya Kristo iliyochorwa humo. Ilikuwa yale mahubiri mlimani. Nayo kwa kweli ilikuwa nzuri sana. Hakika nawashukuru. Na vitu vingi sana, sijui jinsi ya kuwashukuru. Ndiposa, pia kwa—kwa kudhaminia, kugharimia mikutano hii, bila shaka tunawashukuru kwa mioyo yetu yote. Bwana na awabariki kila mmoja wenu sana.

¹⁰ Billy alisema kulikuwa na watu wengi waliohitaji mahojiano ya kibinafsi wakati huu. Na wengi waliomba na walikuwa na watoto wadogo wa kuwekwa wakfu. Lo, jinsi ninavyotaka kufanya hivyo! Lakini mnaona, nilipokuja wakati huu, ni muhimu sana yanipasa kukaa hapa wakati wote katika kusoma Neno hili na kuomba kwa ajili ya kuzileta hizi jumbe. Mwaona, hizi si... Ni—ni geni sana kwetu, kwa sababu ni kutafuta mapenzi ya Mungu na basi kunena mambo haya. Na hayo yote hayana budi kuungana pamoja, na kumuuliza Mungu ni lipi hasa litafunguliwa.

¹¹ Sasa, Bwana akitujalia, tutarudi tena hivi karibuni, mara tu tuwezapo kupata siku. Nilitoa hoja ama—nilisema neno kuhusu Pasaka. Yanipasa nichuguze hilo, kwa sababu nafikiri nina mipango mingine California mnamo wakati huo. Kwa hivyo huenda hiyo ni makosa. Ingawaje, tutakaporudi tena Maskanini,

tutawatumieni kadi na—kanisa, na na kuwapa ninyi—tarehe na wakati.

¹² Ndipo nita... Huenda ikawa wakati huo... Tena sijapanga wakati wo wote wa kuwaombea wagojwa. Hatujapata ibada moja ambayo tuliwaleta watu na kuwaombea. Tumekuwa tukiwaacha waende. Na Ndugu zetu hapa wamekuwa wakihubiri, Ndugu Lee Vayle, na Ndugu... Ndugu hawa wengine wamekuwa wakihubiri na kuombea wagojwa, na kufanya ubatizo wa maji—kubatiza samahani, na kuniachia Neno mimi peke yangu. Tunawashukuru watu hawa. Wamefanya kazi ya heshima sana.

¹³ Kuna marafiki wengi sana hapa ambao ningetaka kukutana nao. Nilitazama kule chini na kumwona John na Earl. Na kuna Daktari Lee Vayle, mmoja wa wasimamizi wa mikutano hii—Ndugu Roy Borders. Watu hao, sina hata—hata sijawaamkua kwa mkono. Sijapata nafasi. Nawaza kuhusu marafiki wangu kutoka Kentucky, na kutoka humu, na marafiki wahudumu, jinsi ningependa kuwasalimia. Ndugu Blair, nilimwona hapa hivi majuzi. Na wengi wa wale watu ni—ninaowapenda; nao wamehudhuria mikutano mingi; sikupata hata kuwasalimia kwa mikono. Ni—ninajaribu... Si eti sitaki kufanya hivyo; ni kwa sababu sina wakati wa kufanya hivyo. Nami naharakisha tu.

¹⁴ Kuwaweka watoto wakfu, naam, mwanangu mimi mwenyewe, mjukuu wangu alihitajiwa kuwekwa wakfu, kwenye mikutano hii. Sijapata wakati wa kufanya hivyo, mtoto Daudi. Mimi ni babu mara mbili sasa. Kwa hivyo Bw. May, iwapo yuko hapa usiku wa leo, aliyenipa ile fimbo, inaonekana sina budi kuitumia hivi karibuni, kwa hivyo...

¹⁵ Nami nilimwambia Billy, nikasema, “Biblia bila shaka ilisema mkaongezeke, mkajaze nchi, bali mzigo huo wote haukupewa wewe.” Na hawa wajukuu wanazaliwa upesi sana. Na sasa kumbukeni, mkwe wangu alikuwa tasa kwanza; hangaliweza kupata watoto. Na siku moja nilipokuwa nikiondoka mkutanoni, Bwana alinena nami na kusema, “Loyce, utamzaa mwana; Bwana amekubariki. Shida yako ya uke imekuacha.” Mtoto Paul akazaliwa miezi sita baadaye.

¹⁶ Miezi miwili kabla mtoto huyu hajazaliwa, nilikuwa nimeketi chini, nikila kifungua kinywa asubuhi moja mezani, naye Loyce na Billy walikuwa wameketi mezani upande mwingine. Nami nikamwona Loyce akimlisha mtoto mchanga akiwa na pinki—au amevikwa blanketi samawati. Naye Billy alikuwa ameketi pembeni akimlisha mtoto Paulo. Nikasema, “Billy, nimeona ono sasa hivi. Loyce alikuwa akimlisha mtoto aliyevikwa blanketi samawati.”

Yeye akasema, “Basi safari yangu ya mawindoni haimo tena. Hiyo ni miezi tisa tu tangu sasa.”

Miezi kumi na moja baadaye maskini Daudi akazaliwa. Bado sijapata nafasi ya kumweka wakfu kwa Bwana, na sitaipata hadi tutakaporudi tena. Kwa hivyo unaona ni nini.

¹⁷ Jinsi nipendavyo watu na ushirika wao. Bali ndugu zetu wamekuwa wakiombea wagojwa, nami najua imefaulu. kila usiku tunawaombea wagojwa, tukiwekeleana mikono sisi sote pamoja, ambapo kwa njia hiyo inaenea kote. Bali huenda ikawa, Mungu akipenda—nitaiandika kwa ile kadi kama tukiituma—nikirudi, ningetaka kutenga siku mbili tatu tena kuombea tu wagojwa na kufanya tuwezavyo hivyo.

¹⁸ Sasa—sasa, nawashukuru watu kwa msaada wao tena. Sasa, nataka tu kufafanua kwa muda mchache tu juu ya—juu ya ule ujumbe wa asubuhi hii. Bila shaka sikuumaliza kabisa, bali naamini mnaelewa. Nami nina hakika hamku. . . Hamtajua kamwe hiyo ilikuwa nini kwangu kutenda.

¹⁹ Naam, inaonekana rahisi sana kwenu bali unaona unalofanya? Unachukua mahali pa Mungu kutangaza jambo fulani. Na kabla sijafanya hayo, ilipaswa jibu litoke kwa Mungu. Naye ilimpasa kushuka, na akajionyesha waziwazi, nakutoa ufunuo huo. Kwa hivyo (mwaona?), hili ni kwa kanisa. Na kumbukeni, nilisema haya—haya niliyosema yalikuwa kwa ajili ya kanisa pekee.

²⁰ Na ili mkapate matumaini na kujua, huyo alikuwa Mungu yule aliyeniambia kule ambako hakukuweco kuchakulo wo wote. “Nena, ukaseme watakakokuwa.” Na mara tatu moja kwa moja ikatendeka. Naam, kama yeye anaweza kwa Neno lilo hilo kuumba kitu kisichokuwepo, ni zaidi vipi hili litasimama imara kwenye ile siku ya hukumu! Mwaona? Watu walikuwa kule kuona mambo haya na kujua, kama Paulo alivyosema siku zilizopita, kuna watu waliokuwa pamoja naye ambao—waliosikia nchi ikitetemeka na hawakuisikia ile sauti, bali wao—waliona ile—ile Nguzo ya moto.

²¹ Ilinifurahisha ingawaje baada ya kuumaliza kuona mabwana na wake zao ambao najua ni Wakristo halisi wakikumbatiana wao kwa wao na kulia. Na sikizeni, marafiki Mungu huthibitisha Neno lake kwa ishara na ushuhuda kuhakikisha ya kwamba ni kweli. Neno lililonenwa!

²² Sasa kumbukeni, ile Nuru iliyokuwa kwenye lile wingu iliyotoa ule ufunuo. . . Nilikuwa. . . Msichana wangu mdogo alikuwa akiniambia, Sara hapa, ya kwamba walipo. . . Ile shule pale Arizona ilikuwa ikitazama kule juu kwenye anga zisizo na mawingu na kuona wingu hili la ajabu, kule mlimani, likienda juu-chini pamoja na moto wa majano uliowaka mle ndani. Mwalimu aliwaruhusu wanafunzi na shule nzima kuondoka na akawaleta kule mbele na kusema, “Mmepata kuona kitu kama kile? Tazameni jinsi—ilivyo?” Kumbukeni, hiyo ndiyo nuru ile ile majano iliyo kwenye ule mwamba! Kwa hivyo ni Mungu yule

yule, ufunuo ule ule. Kasema, “Waambie wafanye hivi”. Ni yale niliyowaambia asubuhi ya leo, na ndiyo hiyo.

²³ Iwapo rafiki msiri wangu Ndugu Roy Roberson anasikiza kule Tucson, Roy, unakumbuka hivi majuzi lile ono uliloona tulipokuwa tumesimama juu ya mlima? Ulinijia, na lile wingu lilikuwa kule juu? Ukashuka, unajua Yeye alivyokwambia, si nilikwambia mle nyumbani hivi majunzi? Ndiyo hiyo Roy. Usijali tena, mwanangu; imekwisha.

²⁴ Hamjui hata kidogo maana yake. Ni neema! Anawapenda! Mpendeni. Mtumikieni na kumwabudu Yeye siku zenu zote. Furahini, endeeleni kuishi mnavyoishi. Iwapo mna furaha, endeeleni vivyo hivyo. Msitende kamwe cho chote kibaya namna hiyo tena. Endeeleni tu; ni neema ya Mungu!

²⁵ Sasa, nataka kuomba tena kabla hatujaingilia Neno. Ni wangapi watakaoniomba? Mimi ninatoka tu kwenye mkutano huu kwenda huu, je, mtaniomba? Mwajua, ningetaka kuwaambia wimbo mdogo, sote pamoja kabla hatujaliendea Neno. Ili tu—ili tupate kumjua, Mungu... Kujiweka wakfu kidogo tu. Je, mmepata kusikia wimbo huu mdogo, *Yeye Anakulinda?* Kwenye nuru na kivulini, yeye hukulinda.

²⁶ Bibi mdogo anakuja kwenye kinanda. Aisee, nataka kumshukuru huyu bibi mdogo pia; hata sikujua alikuwa nani. Alikuwa mmoja wa binti za shemasi hapa. Bila shaka msichana wa Ndugu Wheeler, amekuwa mkubwa sasa. Alikuwa kitoto kichanga kilichoketi magotini mwangu si muda mrefu uliopita, na sasa yeye ni kijana mwanamke. Kwa hivyo bila shaka namshukuru kwa kuwa ametumia kipawa chake cha muziki, na sasa yeye hucheza vizuru sana. Je, unaweza kutupa sauti yake, Dada? Sote pamoja sasa.

Anakulinda;
Anakulinda;
Kwenye nuru na kwenye kivuli
Yeye hukulinda.

Je mnapenda hilo? Hebu na tuimbe tena sote pamoja.

Anakulinda;
Anakulinda;
Kwenye nuru na kwenye kivuli
Yeye hukulinda. (Ndugu Dauch, Yeye hukutendea hayo pia, Ndugu!)

²⁷ Je hamumpendi? Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Mungu mwenye neema, kwa haya maandishi mdogo ya mambo machache ya kuwaambia watu na kurudi tena kutaja tena asubuhi ya leo, kwa maana hayo ndiyo watu huja kusikia. Naomba, Mungu, utawaruhusu watu kuona ya kwamba Mungu awapenda na kuwalinda. Na si mimi niliyetoa hayo Bwana, ilithibitishwa ya kwamba ilikuwa kweli. Hivyo naomba, Mungu mpendwa, ya kwamba upendo Wako daima utadumu miongoni

mwa watu hawa. Usiku wa leo tutahitajika tutengane baada ya mkutano na kuenda nyumbani mwetu mbali mbali, ina—inatutatia, wengine wetu, sana, Bwana. Naomba ya kwamba utawabariki watu hawa.

²⁸ Sasa tunapokaribia Neno kwa maombi, na kuliendea Neno lililoandikwa, tunakuomba ya kwamba utachukua Neno hili lililoandikwa na kulifanya hai kwetu usiku wa leo. Na tunapoondoka kwenye hili jengo kufumukana kwenda nyumbani mwetu mbali mbali, na tuseme kama wale waliokuja toka Emau, waliokuwa wametembea Naye siku nzima na bado hawakumjua... bali alipowaingiza mle chumbani usiku huo, huku milango yote imefungwa, Yeye alitenda jambo fulani jinsi alivyotenda kabla ya kule kusulubishwa Kwake. Kwa tendo hilo wao wakajua ya kwamba Yeye amefufuka. Tenda hivyo tena usiku wa leo, Bwana. Tujalie, huku milango imefungwa na kikundi Chako kidogo kinaketi kikingoja. Baba tufikapo nyumbani mwetu tutasema kama walivyosema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani!” Tunajikabidhi sisi wenyewe na wengine wote mikononi Mwako, Bwana, tenda nasi upendavyo. Katika Jina la Yesu. Amina.

²⁹ Sasa, hebu na tuingie kwenye ibada haraka sasa, mkifungua pamoja nami kama mkipenda kwenye kitabu cha Waebrania. Na ufunuo mwingine juu ya Ujumbe, tutakaounena kwa dakika chache tu usiku wa leo, Bwana akipenda. Na ndipo tunaposoma vifungu vya kwanza vitatu vya Waebrania 7:1-3, na kisha kufafanua haya... Na hatujui Bwana atakayotenda. Hatujui; jambo tufanyalo tu ni kuamini tu, kukesha, kuomba (sivyo?), na kuamini ya kwamba Yeye atafanya mambo yote yafanye kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema kwa sababu aliahidi kufanya hivyo.

Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimamu alipokuwa akirudi kuwapiga hao wafalme; akambariki;

Ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote; tafsiri ya jina la kwanza ni mfalme wa haki, tena, Mfalme wa Salemu maana yake, mfalme wa amani, (Tusome zaidi kidogo.)

Hana baba, hana mama, hana wazazi... hana mwanzo wa siku zake, wa mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu; huyo adumu kuhani milele.

³⁰ Waza kuhusu mtu huyu mkuu, jinsi inampasa mtu huyu kuwa mkuu. Na sasa, swali ni kwamba: “Mtu huyu ni nani?” Wanatheologia wamekuwa na mawazo tofauti, bali tangu kule kufunguliwa kwa zile mihuri saba, kile kitabu cha siri ambacho kimekuwa cha siri kwetu... Kulingana na Ufunuo 10:1-7, siri zote ambazo zimeandikwa kwenye Kitabu hiki ambazo

zimefichwa kote katika zile nyakati za wale warekebishaji zinahitajika kufunuliwa wazi wazi na malaika wa wakati wa mwisho wa kanisa. Wangapi wanajua hayo ni kweli? Naam! Zinahitajika kuletwa. Siri zote za kile Kitabu cha kisiri zitafunuliwa kwa mjumbe wa wakati wa Laodikia.

³¹ Kwa maana kuna ubishi mwingi kuhusu Mtu huyu, na somo hili, nafikiri inatupasa tuliangalie tupate kuona huyu ni nani. Sasa, kuna mafundisho mengi kumhusu yeye. Fundisho moja ni—hudai Yeye ni hadithi tu ya kubuniwa; hakuwa mtu halisi. Na lingine husema kwamba ilikuwa ukuhani, huo ulikuwa ukuhani wa Ki-melkizedeki. Hilo ndilo lina uwezekano zaidi na ambalo linakaribia ukweli kuliko lile lingine, kwa sababu wao husema ilikuwa ukuhani. Haiwezekani, kwa maana katika kifungu cha 4 husema Yeye alikuwa Mtu, Mwanamume. Kwa hivyo ili awe mtu Yeye anapaswa kuwa na utu, Mtu. Si utaratibu fulani, bali Mtu.

³² Kwa hivyo hakuwa tu utaratibu wa ukuhani, wala hakuwa hadithi ya kubuniwa; alikuwa Mtu. Na mtu huyo ni wa milele. Kama ukitazama, Yeye hana baba, hana mama, hana mwanzo wa siku Zake, hana mwisho wa-siku Zake. Na hata awe alikuwa nani Yeye angali hai usiku wa leo, kwa sababu Biblia ilisema hapa ya kwamba Yeye hana baba, wala mama, mwanzo wa siku Zake wala mwisho wa uhai Wake. Kwa hivyo haina budi kuwa ni Mtu wa milele. Sivyo? Mtu wa milele. Kwa hivyo inaweza tu kuwa Mtu mmoja; huyo ni Mungu, maana ni Yeye tu aliye wa milele—Mungu.

³³ Naam, katika 1 Timotheo 6:15 na 16, kama mngetaka kusoma hapo wakati mwingine, ningetaka msome. Sasa, jambo ambalo nasisitiza ni, ya kwamba Yeye alikuwa Mungu, kwa sababu Yeye ndiye Mtu pekee ambaye anaweza kuwa asiyekufa. Na sasa, Mungu aliyejibadilisha Mwenyewe kuwa mtu; hivyo ndivyo alivyokuwa. Hana baba hana mama, hana mwanzo wa uhai Wake, wala mwisho wa siku.

³⁴ Sasa, tunapata kwamba katika maandiko watu wengi hufundisha kwamba kuna nafsi tatu katika Uungu. Kwa hivyo huwezi kuwa na nafsi bila kuwa mtu. Inachukua mtu kufanya nafsi.

Muhudumu Mbaptisiti majuma machache yaliyopita alikuja nyumbani mwangu—na kusema, “Ningetaka kukunyosha kwa Uungu wakati mwingine upatapo nafasi!”—akanipigia simu, samahani.

³⁵ Nikasema, “Nina nafasi hivi sasa, maana nataka kuwa mnyofu, na tutaweka kando kila kitu tufanye hivyo.”

Naye akaja; akasema, “Ndugu Branham, unafundisha ya kwamba kuna Mungu mmoja tu.”

Nikasema, “Naam, bwana!”

Akasema, “Vema,” akasema, “Naamini kuna Mungu mmoja, bali Mungu mmoja katika nafsi.”

Nikasema, “Bwana, rudia hayo tena.”

Akasema, “Mungu mmoja katika nafsi tatu.”

³⁶ Nikasema, “Ulisomea wapi?” Waona? Akaniambia chuo cha Biblia. Nikasema, “Ningeweza kuamini hilo? Huwezi kuwa mtu pasipo kuwa nafsi, na kama wewe una nafsi, wewe ni nafsi mmoja kwako mwenyewe. Wewe ni mtu binafsi peke yako.”

Naye akasema, “Vema, wanatheologia hawawezi hata kueleza hayo.”

Nikasema, “Ni kwa ufunuo.”

Akasema, “Siwezi kukubali ufunuo.”

³⁷ Nikasema, “Basi hamna njia kwa Mungu kuweza kukufikia kamwe, kwa sababu yamefichwa wenye hekima na akili, na kufunuliwa watoto wachanga—kufunuliwa, ufunuo kufunuliwa watoto wachanga walio tayari kuyapokea kujifunza.” Nami nikasema, “Hapangekuwepo njia kwa Mungu kukufikia, umejifungia mbali Naye. Biblia nzima ni ufunuo wa Mungu. Kanisa lote limejengwa juu ya ufunuo wa Mungu. Hamna njia nyingine ya kumjua Mungu ila kwa ufunuo: ‘Kwa yeye yule mwana atakayemfunulia—’ ufunuo. Kila kitu ni ufunuo. Kwa hivyo ku—kutokukubali ufunuo, basi u mwanatheologia aliye baridi, na hamna tumaini kwako.”

³⁸ Sasa, Sasa, tunaona ya kwamba mtu huyu hana baba, wala mama, hana mwanzo wa siku zake wala mwisho wa uhai wake. Ilikuwa ni Mungu *En morphe*. Basi, ulimwengu—lile neno limetoka—kwa neno la Kiyunani maana yake “kubadilika,” lilitumika, kujibadilisha Mwenyewe, *En morphe*, kutoka mtu mmoja kuingia...mtu mmoja...Neno la Kiyunani hapa, *En morphe*, maana yake—lilitolewa kwenye michezo ya kuigiza—“huyo mtu mmoja akibadilisha kinyago chake kujifanya mtu mwingine.”

³⁹ Kama kule—kule shuleni hivi majuzi—naamini, Rebeka, kabla tu hajafuzu—walikuwa na mmoja wa michezo ya Shakespeare. Na kijana mmoja ilimpasa kubadilisha nguo zake mara kadhaa, kwa kuwa alicheza sehemu mbili au tatu mbali mbali—bali mtu yule yule. Akajitokeza; wakati mmoja alikuwa mjeuri. Na alipojitokeza mara ya pili, alikuwa mtu tofauti.

⁴⁰ Na sasa Neno la Kiyunani *En Morphe* maana yake ni kwamba yeye alibadilisha kinyago Chake. Na hivyo ndivyo Mungu alivyofanya. Ni Mungu yule yule wakati wote. Mungu katika mfano wa Baba, yule—yule Roho, ile Nguzo ya moto, Mungu yule yule alifanyika mwili na kukaa kwetu—*En Morphe*, akatolewa apate kuonekana. Na sasa, Mungu yule yule ndiye Roho Mtakatifu. Baba, Mwana, Mtakatifu—sio Miungu watatu, afisi tatu, matendo matatu ya Mungu mmoja.

41 Biblia inasema kuna Mungu mmoja, sio watatu. Bali hivyo ndivyo kwamba hawangeweza... Hauwezi kunyosha haya na kupata miungu watatu. Haungaliweza kumuuzia Myahudi hayo; nakwambia hayo—yule anayejua bora zaidi—anajua kuna Mungu moja tu.

42 Tazama, kama fundi wa kuchonga sanamu za mawe, huifunika kwa—kinyago juu yake. Hivyo ndivyo Mungu ametenda kwa kizazi hiki. Ilikuwa imefichwa. Mambo haya yote yamekuwa yamefichwa, na yamepaswa kufunuliwa katika kizazi hiki. Naam, Biblia ilisema yangefunuliwa wakati wa mwisho. Ni kama huyo fundi akifu—akifunika kazi yake hata wakati atakapoondoa kile kinyago kwake na ikaonekana wazi. Na hivyo ndivyo Biblia imekuwa. Imekuwa kazi ya Mungu iliyofunika. Na imefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, na ni ile siri yenye sehemu saba, Mungu aliahidi katika siku hizi, katika wakati wa kanisa la Laodikia, Yeye angeondoa kile kinyago kutoka kitu hicho chote na tungeweza kukuiona.

43 Ni jambo lenye utukufu jinsi gani! Mungu, *En Morphe*, aliyetiwa kinyago katika Nguzo ya moto, Mungu, *En Morphe* katika mtu aliyetiwa Yesu, Mungu *En Morphe* katika kanisa Lake—Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu, Mungu anayejidhili. Kule juu mtakatifu, hamna angalimghusa; akashuka mlimani. Na hata kama mnyama yeyote angeligusa ule mlima, ilimpasa kufa. Na kisha Mungu akashuka na kubadilisha hema lake, na akushuka chini na akaishi nasi, akawa mmoja wetu na tulimshika-shika Yeye. Biblia ilisema, I Timotheo 3:18, “Bila shaka siri ya uungu ni kuu. Mungu alidhihirishwa katika mwili”—akashikwa-shikwa kwa mikono! Mungu akala nyama. Mungu akanywa maji. Mungu akalala. Mungu akalia. Yeye alikuwa mmoja wetu! Vizuri, imeonyeshwa katika Biblia. Huyu alikuwa Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, sasa ni Mungu ndani yetu, Roho Mtakatifu, si mtu wa tatu, mtu yule yule!

44 Mungu alishuka chini na kufanyika mwili na kufa mauti katika Kristo kusudi apate kusafisha Kanisa apate kuingia ndani yake kwa ajili ya ushirika. Mungu hupenda ushirika. Hilo ndilo alilomuambia mwanadamu mara ya kwanza, ilikuwa kwa ajili ya ushirika. Mungu huishi peke Yake pamoja na Makerubi.

45 Na tazama sasa, Yeye alimfanya mwanadamu, naye mwanadamu akaanguka. Ndipo akashuka chini apate kumkomboa mwanadamu, kwa maana Mungu hupenda kuabudiwa! Neno lenyewe *mungu* maana yake ni “kitu cha kuabudiwa.” Na hii ambayo huja kwetu kama Nguzo ya Moto, ambayo wakati mwingine hugeza mioyo yetu, huyo ni Mungu yule yule aliyesema, “Iwe nuru,” na ikawa nuru. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

⁴⁶ Basi, hapo mwanzo Mungu aliishi pamoja na sifa Zake kama nilivyonena asubuhi ya leo. Hizo ni mawazo Yake. Hapakuwepo kitu, Mungu peke Yake. Bali alikuwa na mawazo. Kama tu vile mjenzi mashuhuri aweza kutayarisha, niani mwake, na kuchora anachowaza kita—ata—atajenga, kuumba. Sasa, hawezi kuumba; anaweza kuchukua kitu kilichoumbwa na kukitengeneza vingine, maana Mungu ndiye njia pekee—mtu pekee anayeweza kuumba. Bali anawaza niani Mwake atakayotenda, na hayo ni mawazo Yake, hayo ni matakwa Yake.

⁴⁷ Sasa, ni wazo, kisha analinena, na ndipo ni neno basi. Na ne—neno ni...wazo linapotamkwa, ni neno. Wazo linapotamkwa ni neno. Bali haina budi kuwa wazo kwanza. Ndivyo zilizvyo sifa za Mungu; kisha zinakuwa wazo, halafu neno.

⁴⁸ Tazama, wale walio na uzima wa milele usiku wa leo, walikuwa pamoja Naye na ndani Yake, katika mawazo Yake, kabla hapajakuwepo malaika, nyota, kerubi, ama cho chote kile. Huo ni umilele. Na iwapo una Uzima wa Milele, ulikuwako daima. Si kuweko kwako hapa, bali umbo na mfano ambao Mungu asiye kikomo...kama Yeye si asiyo kikomo; Yeye si Mungu.

⁴⁹ Mungu hana budi kuwa asiye kikomo. Sisi tuna kikomo; Yeye hana kikomo. Naye alikuwa aliye mahali pote, ajuaye yote, na mwenye nguvu zote. Kama sivyo alivyo basi Yeye si Mungu. Anajua mambo yote, mahali pote kwa sababu ya kuenea Kwake mahali pote. Kujua yote humfanya aliyekeo kila mahali. Yeye ni kiumbe; si kama upepo. Yeye ni kiumbe; huishi katika nyumba, bali kwa ajili Yeye ni mjua yote, anayejua vitu vyote, inamfanya aliyeenea kote kwa maana anajua mambo yote yanayotendeka. Hapawezi kuwepo kiroboto anayefunga jicho lake bila Yeye kujua. Na alijua kabla ulimwengu haujakuwepo, ni mara ngapi kingefunga macho yake na kina shahamu kiasi gani ndani yake, kabla hapajakuwepo ulimwengu. Hiyo ni isiyo kikomo. Hatuwezi kuelewa kwa akili zetu. Bali huyo ni Mungu—Mungu, asiye kikomo.

⁵⁰ Na kumbuka, wewe, macho yako, umbo lato, cho chote ulichokuwa, ulikuwa katika mawazo Yake hapo mwanzo. Na kitu tu wewe ulicho ni dhihirisho tu la neno. Alipoliwaza, akalineni, nawe ndiye huyo. Kama sivyo, kama haukuweko katika mawazo Yake, hamna uwezekano kamwe kwako kuweko kule, kwa maana Yeye ndiye anayetoa uzima wa milele.

⁵¹ Mnakumbuka tulivyosoma yale Maandiko, “Si katika uwezo wa yule atakaye, wala wa yule apigaye mbio, bali Mungu. . .” Na ili kwamba kuchagua Kwake kimbele kusimame angelichagua kabla ya wakati wo wote yule...Mungu ni mwenye enzi katika kuchagua Kwake, mlijua hayo? Mungu ni mwenye enzi. Je, nani aliyekuweko kule nyuma kabisa kumwambia njia bora

ya kuufanya ulimwengu? Nani awezaye kuthubutu kumwambia anaendesha kazi Yake vibaya? Hata lengo—Neno Lenyewe, lina mamlaka. Hata ufunuo una mamlaka. Yeye humfunulia anayetaka kumfunulia. Ufunuo wenyewe ni mamlaka ya Mungu. Hivyo ndivyo watu wanaponda—ponda, na kurukia vitu, na kupiga vitu, na bila kujua watendavyo. Mungu ana mamlaka juu ya kazi Zake.

⁵² Sasa, tunamwona hapo mwanzo, sifa Zake. Na sasa, ulikuwa pamoja Naye wakati huo. Hapo ndipo kile Kitabu cha Uzima kinapoonekana wazi. Sasa tunasoma hapa katika Ufunuo sura ya 13, kifungu cha 8, ya kwamba yule mnyama atakayekuja juu ya nchi katiaka hizi siku za mwisho atawakosesha watu wote wakao juu ya nchi ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha mwana Kondoo tangu kuwekwa misingi ya dunia.

⁵³ Wazia hilo! Kabla Yesu hajazaliwa kamwe, miaka elfu nne kabla hajakuja duniani, na miaka elfu kadhaa kabla hujakuja duniani, Yesu katika mawazo ya Mungu alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwingu, na kile Kitabu cha Uzima kikatengenezwa; na jina lake likawekwa kwenye hicho Kitabu cha Uzima tangu kuwekwa misingi ya dunia! Huo ni Ukweli wa Biblia. Waona? Jina lako liliazimiwa na Mungu na kuwekwa kwenye Kile Kitabu cha Uzima tangu kuwekwa misingi ya dunia.

⁵⁴ Ulikuwa kule katika sifa Zake. Hauwezi kukumbuka, la, kwa sababu wewe ni sehemu tu ya uhai Wake. Wewe ni sehemu ya Mungu unapokuwa mwana wa kiume ama wa kike wa Mungu, jinsi tu wewe ulivyo sehemu ya baba yako wa duniani. Hiyo ni kweli! Wewe ni . . . Mwanamme ndiye hubeba ile chembechembe nyekundu damuni. Nayo inapoingia—kwenye lile yai, ndipo unakuwa sehemu ya baba yako, na mama yako ni sehemu ya baba yako pia. Kwa hivyo ninyi nyote ni sehemu ya baba yako. Utukufu! Hilo huondoa dhehebu nje kabisa. Hakika hufanya hivyo! Mungu ndani ya yote mahali pekee.

⁵⁵ Tazama sasa sifa Zake. Ndipo zile sifa kwanza zilikuwa Mungu, wazo, sifa zenyewe, zote katika mmoja, bila kutamkwa. Ndipo alipozitamka, jambo la pili, Yeye akawa lile Neno. Ndiposa lile Neno likafanyika mwili na kukaa kwetu. Mt. Yohana mlango wa 1 na kifungu cha 1.

⁵⁶ Tazama, hii ni hapo mwazo, bali hapo kabla ya milele. Tazama, hapo mwanzo kulikuwako Neno. Wakati ulipoanza lilikuwa Neno, bali kabla halijakuwa Neno, lilikuwa sifa, wazo. Kisha likatamkwa. Hapo mwazo kulikuweko kutamkwa, Neno. Sasa, tunafikia alipo Melkizedeki. Huyu ndiye Mtu huyu wa ajabu. Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Na ndipo Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu . . . Shikilia hilo hapo sasa.

57 Tazama, u—umbo Lake la kwanza lilikuwa Roho, Mungu, wa kimbinguni (sivyo?) Yule Umilele mkuu. Pili, yeye akaanza kufanyika mwili wa kiungu—*theophany*, uitwao, “neni, mwili.” Hii basi ndiyo hali aliyokuwamo alipokutana na Ibrahimu, aliitwa Melkizedeki. Alikuwa katika umbo la *theophany* mwili wa kiungu. Sasa, tutafikia hilo na kulithibitisha katika dakika chache, Bwana, akipenda.

58 Yeye alikuwa neno. *Theophany*—mwili wa kiungu—ni kitu ambacho hungeweza kukiona. Kingekuwa hapa sasa hivi, bali hauwezi kukiona. Ni kama tu, vema, kama televisheni, hiyo imo kwenye kiwango kingine. Televisheni... Watu wanapita-pita sasa hivi humu chumbani wakiimba; rangi pia, bali macho yanatawaliwa na zile hisi tano. Utu wako wote unatawaliwa na zile hisi tano, samahani. Nawe unatawaliwa tu na kile macho yawezacho kuona. Bali kuna kiwango kingine kinachoweza kuonekana kwa mawasiliano ya televisheni.

59 Naam, televisheni haitengenezi picha. Televisheni huiongoza tu kwenye mitambo ya spaki, na ndipo kile kioo cha televisheni kinaichukua. Bali picha sharti iweko kwanza. Televisheni ilikuwa hapa Adamu alipokuwepa hapa. Televisheni ilikuwako Eliya alipoketi kwenye mlima wa Karmeli. Televisheni ilikuwako Yesu wa Nazareti alipotembea kwenye pwani za Galilaya. Bali mmeanza tu kuigundua sasa. Hawangaliadini zamani zile. Ungelikuwa mwenda wazimu kama ungalisema kitu kama hicho. Bali sasa imekuwa ukweli. Na vivyo hivyo Kristo yuko hapa! Malaika wa Mungu wako hapa! Na siku moja katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu moja unaokuja itakuwa halisi zaidi ya televisheni ama cho chote kile, kwa maana wako hapa!

60 Yeye hujifunua Mwenyewe katika umbo Lake kuu la yale anayodai anapoji—En Morphe Mwenyewe katika watumishi Wake na kujithibitisha Mwenyewe.

61 Naam, yupo hapa katika umbo la Roho. Ndiposa Yeye huja katika umbo la—la—En Morphe. Basi, alimtokea Ibranimu *En Morphe*. Ibrahimu alipokuwa akirudi kutoka kumpiga mfalme, hapa akaja Melkizekeki, akanena naye.

62 Hivi majuzi katika gazeti la Tucson nilikuwa nikisoma nakala ambapo kulikuwepo mwa—mwanamke aliyeendesha motokaa barabarani, yapata naadini mwendo wa maili arobaini, au hamsini kwa saa, naye akamgonga mzee mwenye kabuti. Mwanamke huyo akapiga mayowe na kusimamisha motokaa yake. Ilimrusha huyo mzee hewani. Moja kwa moja jangwani! Naye akakimbia nyuma kumtafuta naye hakupatikana. Kwa hivyo akafanyaje? Watu wengine nyuma yake waliona hayo yakitendeka, kamwona yule mzee akirushwa hewani, kabuti lake likepeperuka. Ndipo wakakimbia kule nyuma kumtafuta. Hawakumpata yule mtu mahali po pote.

Wakawaita polisi. Polisi wakaja kuchunguza mahali pale; hapakuwepo mtu pale.

⁶³ Vema, kila mmoja wao alishuhudia ya kwamba ile motokaa ilitikisika, ikamgonga yule mtu. Akarushwa hewani, na kila mtu aliona hayo. Mashahidi, na walijaa motokaa mbili tatu, waliona ikitendeka. Ikagunduliwa baadaye, kumbe! Miaka mitano iliyopita kulikuwako mzee mmoja mwenye kabuti aliyegongwa na kuuawa pale pale. Unapoondoka hapa, haujaangamia bado. Huna budi kurudi tena hata ikiwa wewe ni mwenye dhambi na uhukumiwe kulingana na matendo yaliyotendwa katika mwili. “Nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo nyingine inayotungoja”. *En Morphe*, hiyo ni Neno.

⁶⁴ Sasa Mungu katika sehemu— sehemu hii ya uumbaji Wake baadaye akamfanya Yesu mwili. Kutoka kwa nini? Kutoka ile Roho kuu ya hapo mwanzo, ndipo akashuka kuwa Neno, akijitoa nje. Neno halijifanyi Lenyewe, hunenwa tu *En Morphe*, hatimaye Yeye akafanyika mwili, Yesu, mwenye kufa kusudi akaonje mauti kwa ajili yetu sisi sote wenye dhambi.

⁶⁵ Ibrahimu alipokutana Naye, alikuwa Melkizedeki. Yeye anaonyesha dhahiri hapa jinsi zile sifa zote zitakavyofanya mwishoni, kila mwana wa Ibrahimu. Kila mwana wa ile imani bila shaka atafanya vile vile. Bali ninataka kuangalia jinsi itupasavyo kuja.

⁶⁶ Pia tunamwona amefunuliwa hapa katika Ruthu na—na Boazi kama mkombozi wa jamii yetu, jinsi ilimpasa kuja katika mwili.

⁶⁷ Sasa, tunaona zile sifa, wana wa Roho Wake hawajaingia bado katika umbo la mwili wa Neno, lakini—theophany—mwili wa kuingu. Huu mwili uko chini ya mamlaka ya Neno na arabuni—ukingojea arabuni ya kubadilishwa kwa mwili.

⁶⁸ Basi, tofauti kati Yake na wewe kama mwana... Unaona, Yeye alikuwa hapo mwanzo neno, mwili *En Morphe*. Akaingia na kuishi mwilini huo wa kiungu katika Utu wa Melkizedeki. Ndipo baadaye... Hatukusikia tena habari za Melkizedeki, kwa sababu Yeye alifanyika Yesu Kristo. Melkizedeki alikuwa yule Kuhani, bali akafanyika Yesu Kristo. Basi, wewe uliruka hilo, kwa kuwa katika umbo hilo Yeye alijua yote. Nawe haujapata kujua hayo bado. Ulikuwa kama Adamu, kama mimi. Ulitoka kwenye zile sifa ukafanyika mwili upate kujaribiwa. Bali maisha haya yakwishapo hapa... “Nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo nyingine inayotungoja.” Hapo ndipo tunapokwenda; hiyo ni Neno. Ndipo tunapoweza kutazama nyuma na kuona yale tumetenda. Sasa hatuelewi hayo. Hatujapata kuwa Neno kamwe: tumekuwa tu mtu mwenye mwili, si Neno. Bali...

⁶⁹ Na tazama kwa makini, inakuonyesha wazi ya kwamba hautakuwa Neno kamwe isipokuwa ulikuwa wazo hapo

mwanzo. Hiyo inathibitisha kule kuchaguliwa kimbele kwa Mungu. Unaona? Hauwezi kuwa Neno isipokuwa wewe ni wazo. Ilikupasa kuwa katika mawazo kwanza. Lakini waona, ili kustahimili majaribio, ilikubidi kuruka ule mwili wa kiungu; ilikupasa kuja humu chini katika mwili ukajaribiwa na dhambi. Ndiposa ukitenda dhambi... “Wote alionipa Baba yangu watanijia mimi, nami nitamfufua katika siku za mwisho.” Unaona, ilikupasa uwe hivyo kwanza. Na ndipo unaona, Yeye alishuka moja kwa moja kupitia njia ya kawaida, kutoka kwenye sifa kuingia...

⁷⁰ Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu jina lake liliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha mwana-kondoo. Ndipo kutoka humo akawa Neno, ule mwili wa kiungu, ambao ungeonekana, ukatoweka; na ndipo akafanyika mwili na kurudi tena, akaufufua mwili uo huo katika hali ya utukufu. Bali wewe ulipita ule mwili wa kiungu na kufanyika mwanadamu wa mwili kusudi ukajaribiwe kwa dhambi. Ndipo basi “nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa tuna nyingine inayotungoja.” Hatuna bado ile miili. Bali tazameni, mwili huu unapompokea Roho wa Mungu, ule uhai usiokufa ndani yako, unatiisha mwili huu chini ya Mungu. Haleluiya!

⁷¹ “Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; hawezi kutenda dhambi.” Warumi 8:1 “Sasa, basi, hakuna hukumu ya dhambi juu yao walio katika Kristo Yesu: hawafuati mwili bali Roho.” Ndivyo hivyo! Unaona, hiyo huutiisha mwili wako. Haikupasi kusema, “Jamani, laiti ningaliacha kunywa pombe, laiti ningali...” Ingia tu katika Kristo; yote imekwisha! Waona, waona? Kwa sababu mwili wako u chini ya mamlaka ya Roho. Hauko tena chini ya mambo ya dunia; yamekufa. Yamekufa; dhambi zako zimezikwa katika ubatizo; nawe u kiumbe kipya katika Kristo. Nao mwili wako unatiishwa chini ya Roho, na kujaribu kuishi; maisha mazuri...

⁷² Kama ninyi wanawake mnaodai eti mna Roho Mtakatifu na huku mnatembea mmevalia suruali fupi na kadhalika, mwawezaje kufanya hivyo? Roho wa Mungu ndani yenu angewezaje kamwe kuwakubalieni kufanya jambo kama hilo? Haiwezekani. Hakika haiwezekani! Yeye si Roho mchafu; ni Roho Mtakatifu.

⁷³ Na ndipo mnapotiishwa chini ya Roho huyo, inatiisha utu wako wote chini ya Roho huyo. Na huyo Roho si kinele ulimwenguni ila hili Neno Mbegu lililodhihiriswa, au lililohuishwa (Haleluya), lililofanywa hai. Na Biblia iliposema, “Usitende hili,” mwili huo unaligeukia upesi; hamna swali. Na ni nini? Ni arabuni ya ufufuo. Mwili huu utafutuliwa tena, kwa sababu tayari umeanza. Ulikuwa wakati mmoja katika hali ya dhambi, matope, uharibifu, bali sasa una arabuni; unaelekezwa kwa yaki mbinguni. Sasa, hiyo ni arabuni kwamba utanyakuliwa, ni arabuni.

⁷⁴ Mtu mgojwa anapolala akifa, hamna kilichobakia isipokuwa kifo, hayo tu ndiyo yanayoweza kutendeka. Nimeona vivuli vya watu walioliwa na kansa pamoja na kifua kikuu, na kuwaona watu hao baadaye wakiwa wazima na wenye nguvu. Kama hamna uponyaji wa kiungu basi hamna ufufuo, sababu uponyaji wa kiungu ni arabuni ya ufufuo. Amina!

⁷⁵ Unajua arabuni ya pesa ni nini, sivyo? Ni malipo ya kwanza! “Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.”

⁷⁶ Tazama, ilivyo ya ajabu, tunampenda. Naam, mwili huu umetiishwa chini ya Roho. Hatujaingia bado katika umbo la Neno, bali tungali katika umbo la mwili, uliotiishwa Neno. Kifo katika mwili kitatupeleka pale.

⁷⁷ Jambo lile lile tu. Waza kuhusu mtoto mchanga. Waweza kumchukua mwanamke, haijalishi ni mwovu vipi, anapokuwa na mimba na anakaribia kupata mtoto, mtazame kabla huyo mtoto hajazaliwa, sijali yule mwanamke ni katili vipi, yeye anakuwa mpole sana. Mna kitu kwake kinachoonekana kitauwa sana, kuona maskini mama akikaribia kuwa mama kwa kupata mtoto. Ni kwa nini? Mwili huo mdogo... Sasa, haujakuwa hai bado. Waona, kitu ulicho tu, ni nyama na misuli. Huko kurukaruka kudogo, hiyo ni misuli inayovuta-vuta. Bali unapotoka kwenye tumbo la uzazi, Mungu huupulizia pumzi ya uhai ndani yake. Na ndipo analia. Mnaona, kama tu—hakika kama kunao mwili wa kawaida, unaotengenezwa, kunao mwili wa kiroho tayari kuupokea mara unapofika hapo.

⁷⁸ Ndipo mtu anapozaliwa mara ya pili kutoka ulimwenguni, yeye anakuwa mtoto mchanga wa rohoni katika Kristo. Na ndipo joho hili la mwili linapobwagwa chini, kunao mwili wa kawaida, mwili wa kiungu—mwili ambao haukujengwa kwa mikono, wala kuzaliwa na mwanamke—ambamo tunaingia. Ndipo huo mwili unarudi huku na kuchukua mwili uliotukuzwa. Hiyo ndiyo sababu Yesu alienda kuzimuni alipokufa na kuwahubiri nafsi waliokaa kifungoni. Akarudia ule mwili wa kiungu. Jamani, ajabu sana! Mungu ashukuriwe!

⁷⁹ II Korintho 5:5 “Mwili wetu ulio wa dunia hii ukiharibiwa (maskani haya ya dunia hii), tunalo jengo lingine.” Mwaona, tumeruka hilo tukaja moja kwa moja kutoka kwa Mungu, zile sifa, kufanyika mwili tukashawishiwa na kujaribiwa kwa dhambi kama Adamu alivyofanywa. Bali kujaribiwa kwa Neno Lake kutakapokwisha, ndipo tutakapochukuliwa kwenye mwili tuliotayarishiwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ni Neno pale tuliloruka na kuja moja kwa moja chini huku tupate kushawishiwa na kujaribiwa. Kama tungalipitia kule, hakungekuweko majaribio; tungalijua mambo yote. Hiyo ndiyo sababu Yesu alijua mambo yote, sababu alikuwa Neno kabla hajafanyika mwili.

⁸⁰ Kisha tunakuwa Neno. Hapa tunaumbwa kwa sura ya Neno tupate kuwa washiriki wa Neno, tuwe washiriki wa Neno, tule Neno, kwa kuchaguliwa kimbele tangu mwanzo. Waona, hiyo cheche ndogo ya uhai ilikuwa ndani yako tangu mwanzo ulipoanza safari yako... Wengi wenu mnaweza kuikumbuka. Mlijiunga na kanisa hili na kujiunga na kanisa lile na kujaribu hili na lile; hamkutosheka. Hiyo ni kweli! Bali siku moja ukalitambua tu. Bila shaka!

⁸¹ Usiku uliopita nilikuwa nikifundisha mahali fulani—naamini ilikuwa kule California, ama Arizona—kama... Naamini nimehadithia hadithi hiyo ndogo hapa kuhusu mtu aliyemwatimisha kuku yai la tai. Na yule tai alipoanguliwa, alikuwa ndege wa kuchekeka sana ambaye vifaranga hao walipata kumwona. Bali akazunguka huku na huko; alikuwa—alikuwa—alikuwa mwenye sura baya zaidi miongoni mwao, kwa maana hangalielewa kamwe jinsi huyo kuku angelia na kukwaruza kwenye zile taka na kula. Hangalielewa. Angesema, “Njoo humu ukale mlo, kipenzi!” Vema, yeye—yeye alikuwa tai; yeye hakula hivyo kamwe. Hakikuwa chakula chake.

⁸² Kwa hivyo angewawinda parare na kadhalika, mwajua, na kuwaita wale vifaranga. Nao vifaranga hao wote wangeenda, wakilialia, na kula. Bali yule maskini kifaranga wa tai hangaliweza. Haikuonekana—haikuonekana sawa kwake.

⁸³ Kwa hivyo siku moja mama yake alikuja kumtafuta. Naye angesikia huyu kuku akilia. Naye angejaribu awezavyo kulia hivyo, bali hangaliweza. Alijaribu kulia kama vifaranga wa kuku lakini hakufaulu. Waona, yeye alikuwa tai. Hapo mwanzoni alikuwa tai. Yeye alianguliwa tu chini ya kuku. Hivyo ni kama wafuasi wengine wa kanisa. Kila... Hivyo ndivyo ilivyo; huwa ni mmoja miongoni mwa kundi nzima aliye kweli.

⁸⁴ Bali siku moja mamake alipuruka juu yao na kulia kwa sauti kuu. Yeye akaitambua. “Hiyo yasikika sawa!” Kwani? Yeye chanzo chake ni tai. Hivyo ndivyo ilivyo kwa Injili, au Neno, uwezo wa Yesu Kristo; mtu anapochaguliwa kimbele kwa Uzima wa Milele, yeye husikia huo mlio halisi, mlio wa Mungu, hamna kinachoweza kumwondoa kwake. Kanisa huenda likasema, “Siku za miujiza zimekwisha, kidoko, kidoko, kidoko! Simama hapo ukale hiki, na simama hapo upate kula kile.”

⁸⁵ Huo uchafu wa ghala hautamfaa tena! Ameondoka! “Mambo yote yanawezekana!” Yeye anaruka. Hiyo ndiyo shida ya Wakristo wengi siku hizi; hawawezi kuinua miguu yao ardhini; yule mama mzee akasema, “Mwanangu, ruka; wewe ni tai. Njoo humu niliko mimi.” Yeye akasema, “Mama, sijawahi kuruka maishani mwangu.”

⁸⁶ Akasema, “Vema, ruka; chanzo chako ni tai; wewe si kuku.” Kwa hivyo akaruka kwa mara yake ya kwanza na kutapatapa mabawa yake; hakufaulu sana, bali aliondoka ardhini. Hivyo

ndivyo tunavyofanya; tunamkubali Mungu kwa imani kwa Neno lililoandikwa. Mna kitu mle. Waona, huo Uzima wa Milele, ulichaguliwa kimbele kwake.

⁸⁷ Babu na nyanya yake walikuwa tai; alikuwa tai kule nyuma kote. Tai hawachanganyikani na mambo mengine. Yeye si kitu kilichochanganyikana mbegu kamwe; yeye ni tai.

⁸⁸ Kisha baada ya kutambua kwamba Neno la Mungu lilikuwa Chakula cha Tai, basi ukaacha mengine. Basi Umeumbwa kuwa mfano halisi ulio hai wa Mungu Aishiye. Ulisikia kutoka kwa mwili wako wa kiungu. “Mwili wetu ulio wa dunia hii ukiharibiwa, tuna mwingine unaotungoja.” Unasema, “Je, hiyo ni kweli, Ndugu Branham?” Naama, hebu na tuchukue tai wachache na kuwatazama kwa muda mchache.

⁸⁹ Kulikuwako jina—mtu jina lake Musa. Kila mmoja anajua ya kwamba nabii huitwa tai katika Biblia. Kulikuwako nabii aliyeitwa Musa. Na siku moja Mungu akamwita—Naye hangalimkubalia akaingie nchini—naye aka—alifia kwenye mwamba. Malaika wakamchukua wakamzika. Kulikuwa na mtu mwingine, tai—, haikumpasa hata kufa. Yeye alivuka Yordani, na Mungu akamtumia gari la farasi na: “Joho hili la mwili alilibwaga chini na akainuka na kupata dhawabu ya milele.” Miaka mia nane baadaye—miaka mia nane baadaye kwenye mlima wa kugeuziwa hapa walisimama hao watu wawili. Mwili wa Musa ulikuwa umeoza kwa mamia ya miaka, bali alikuwa hapa katika umbo hata Petro, Yakobo, na Yohana walimtambua. Amina! “Kama nyumba ya maskani yetu yaliyo ya dunia hii yakiharibiwa...” Kama wewe ni sifa ya Mungu iliyodhihirishwa hapa duniani, una mwili unaokungoja baada ya kuacha ulimwengu huu. Wao wasimama juu ya mlima wa kugeuziwa katika miili yao ya kiungu, kwa maana walikuwa manabii waliojiliwa na Neno la Mungu.

⁹⁰ Pia, hebu tumtazame nabii mwingine wakati mwingine jina lake Samweli. Alikuwa mtu mkuu. Alikuwa amewafundisha Israeli, akawaambia haiwapasi kuwa na mfalme. Akasema, “Je, nimepata kuwaambia jambo kwa jina la Bwana ila lile lililotimia?”

Wakasema, “La, kila jambo ulilosema katika jina la Bwana lilitimia.”

⁹¹ “Yeye alikuwa nabii. Naye akafa. Yapata miaka mitatu au minne baadaye, mfalme akapata shida; hapo ni kabla damu ya Yesu Kristo haijamwagika bado. Alikuwa peponi. Na mchawi wa Endoni akampandishia mtu, kumfariji Sauli. Na yule mchawi alipomwona amesimama, akasema, “Naona Mungu akitoka katika nchi.” Huku mtu huyu amekufa, kazikwa, na kuozea kaburini, huku amesimama pale kwenye pango lile amevikwa joho lake la kinabii, naye alikuwa bado yu nabii. Amina!

⁹² Kwa kuwa alisema, “Mbona umeniita usingizini mwangu, nawe umekuwa adui wa Mungu?” Mtazame akitoa unabii. “Usiku wa kesho utakuwa pamoja nami.” Yeye alikuwa yungali nabii, ijapokuwa alikuwa ametoka katika mwili huu. Mwaona, akaja hapa na alikuwa sehemu ya Neno hilo, naye akatoka kwenye uhai wa mwili huu akaingia katika mwili aliotengenezewa kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu. Akaingia kwenye ule mwili wa kiungu ambao ulikuwa Neno. Mnaelewe? Humo ndimo waumini wote huenda tunapotoka humu.

⁹³ Ndipo katika umbo hilo ule utaji umeinuliwa. Unaona wewe ni neno pia unapoingia mle. Kama mtoto mchanga nilivyosema muda mfupi uliopita. . .

⁹⁴ Sasa tazama. Bwana asifiwe kwa ajili ya kufunuliwa kwa mihuri ndilo ombi langu, kujua mambo haya.

⁹⁵ Sasa, ule ufunuo wa kweli wa Melkizedeki unakuwa wazi—alikuwa Mungu, lile Neno, kabla hajafanyika mwili, Mungu Neno. Hakika ilimpasa kuwa hivyo; hamna mwingine angalikuwa asiyekufa kama Yeye. Mwaona, nilikuwa na baba na mama, wewe pia. Yesu alikuwa na baba na mama. Lakini mtu huyu hakuwa na baba wala mama. Yesu alikuwa na mwanzo wa siku Zake; mtu huyu hana. Yesu alitoa uhai Wake, Mtu huyu hangeweza, kwa sababu Yeye alikuwa Uzima. Na ni mtu yule yule wakati wote. Natumai Mungu atakufunulia hayo. Mtu yule yule wakati wote.

⁹⁶ Tazama cheo Chake, Mfalme wa haki. Sasa, Waebrania 7:2, Mfalme wa haki na Mfalme wa amani. Yeye ni wafalme wawili. Tazama sasa! Waebrania 7:2, Mfalme wa haki, pia Mfalme wa amani. Yeye ni wafalme wawili hapo. Sasa, kwa kuwa alikuja katika mwili na mwili wake wa utukufu ukatwaliwa kule juu, katika Ufunuo 21:16 Yeye anaitwa Mfalme wa Wafalme. Yeye ni wote watatu pamoja. Mnaona? Mfalme Mungu, Mfalme mwili wa kiungu, mfalme Yesu, Yeye ni Mfalme wa Wafalme. Yote imeunganishwa, kama tu ilivyo nafsi, mwili, na roho. Zote hufanyika mmoja.

⁹⁷ Pia yeye ni Baba, ambalo lilikuwa la kwanza, Mwana, na Roho Mtakatifu, yule Roho. Mfalme wa haki, sifa ya Roho; mwili wa kiungu, Mfalme wa—wa amani, mwili wa kiungu, na katika mwili alikuwa Mfalme wa Wafalme—mtu yule yule.

⁹⁸ Wakati ule mwili wa kiungu. . . Musa alipomwona, Kutoka 32, alikuwa katika mwili wa kiungu. Musa alitaka kumwona Mungu. Alikuwa tayari amesikia sauti Yake, akamsikia akinena naye, akamwona pale kwenye kijiti pamoja na Nguzo kubwa ya Moto. Naye akasema, “Wewe ni nani, nataka kujua U Nani?” Musa akasema, “Nitaweka—ukiniruhusu nikuone Wewe. . . nigetaka kuona uso Wako.”

⁹⁹ “Yeye akasema, hapana mtu asiyeweza—kuona uso Wangu,” Akasema, “Nitaweka mkono Wangu machoni pako, nami nitapita. Ndipo unaweza kuona mgongo Wangu, bali si uso Wangu.” Mwaona? Na alipofanya hivyo, Ulikuwa mgongo wa mwanadamu; ilikuwa ule mwili wa kiungu. Ndipo neno lililomjia Musa, Mimi Niko; hilo lilikuwa Neno. Neno lilimjia Musa katika umbo la Nguzo ya Moto katika kijiti kilichowaka moto, MIMI NIKO.

¹⁰⁰ Kama Neno kutoka kwa theologia—kutoka kwa theophany, samahani, Yeye alimjia Ibrahimu kama mwanadamu chini ya mwaloni. Naam, tazama hapo.

¹⁰¹ Kukaja mtu kwa Ibrahimu—watatu—na wakaketi chini ya mwaloni, hao watatu. Na tazama, baada ya kumzungumzia Ibrahimu... Kwa nini Yeye akaja? Ibrahimu, maana alikuwa ndiye mwenye ile ahadi pamoja na ujembe wa kujiliwa na mwana, na pia alikuwa nabii wa Neno la Mungu aliyekuwa akiamini Neno la Mungu, akiyataja yale yaliyokuwa kinyume kama kwamba si kinyume... Mwaona jinsi Neno lilivyo kamilifu? Neno lilimjia nabii. Mwaona, Mungu alikuwa hapo katika mwili wa kiungu, na Biblia ilisema Neno huja kwa nabii. Na Ne—Neno lilikuwa hapo katika mwili wa kiungu...

¹⁰² Sasa, unasema, “Huyo alikuwa Mungu?” Ibrahimu alisema alikuwa. Alisema Jina Lake lilikuwa... Alimwita Yeye *Elohim*. Na, katika mwanzo utaona, “Hapo mwanzo *Elohim* aliumba mbingu na nchi.” Katika mwanzo 18 tunaona kwamba—ya kwamba Ibrahimu aliita Mtu huyu aliyeketi pale na kuna naye, na angeweza kumwambia siri za moyo wake, kumwambia Sara alivyokuwa akiwaza nyuma Yake, Ibrahimu alisema, “Ilikuwa *Elohim*.” Alikuwa katika umbo la mwili wa kiungu. Mnaelewa?

¹⁰³ Tazama baada... Sasa, tunaona ya kwamba Yeye wakati huo alikuwa katika umbo la mwili wa kiungu. Akamwita, “Bwana Mungu, *Elohim*.” Sasa, katika mwanzo 18 tunaona ya kwamba hiyo ni kweli.

¹⁰⁴ Sasa tazama, Ibrahimu... Walikuwa watatu pamoja, bali Ibrahimu alipowakuta hao watatu, alisema, “Bwana Wangu!” Bali Lutu kule chini Sodoma, wawili wao wakashuka kwenda kule; naye Lutu akaona wawili wao wakija, naye akasema, “Bwana zangu!” Mwaona, ilikuwa nini? Jambo la kwanza Lutu hakuwa nabii (hiyo ni kweli!), wala hakuwa mjumbe wa wakati huo. Kwa hivyo yeye hakuwa na ufunuo wake. Bila shaka! Lutu angaliwaita “Mabwana,” dazani yao, angalisema pia “Mabwana,” bali haijalishi Ibrahimu aliona wangapi, ilikuwa ingali Bwana mmoja. Huyu ni Mungu; huyu ni yule Melkizedeki.

¹⁰⁵ Tazama, baada ya vita kwisha Melkizedeki akamwadalia mtoto Wake mshindi Ushirika (wazia hilo!), sehemu Yake Mwenyewe. Sasa, tunataka kuona hapa, katika mfano hapa

ushirika unaonekana hapa. Baada ya vita akajitoa Mwenyewe, kwa sababu ushirika ni sehemu ya Kristo. Na baada ya mashindano kwisha, baada ya kupigwa vikali sana, ndipo unashiriki Kristo, unakuwa sehemu ya Kiumbe hiki. Unaelewa?

¹⁰⁶ Yakobo alipiga miereka usiku kucha na hangemwachilia aende hata alipombariki. Hiyo ni kweli! Vita vya maisha. Na baada ya vita kwisha, ndipo Mungu anakushirikisha sehemu Yake Mwenyewe. Huo ndio ushirika Wake kweli. Ule mkate mdogo na mwembamba huwaakilisha hiyo tu. Haupaswi kushiriki isipokuwa umepigana vilivyo na umekuwa sehemu ya Mungu.

¹⁰⁷ Kumbukeni, wakati huu ushirika haukuwa umeanzishwa, si hadi kabla—kifo cha Yesu Kristo, mamia na mamia na mamia ya miaka baadaye.

¹⁰⁸ Bali Melkizedeki baada ya mtoto wake Ibrahimu kupata ushindi, Melkizedeki alimlaki na akampa divai na mkate, ikionyesha ya kwamba baada ya vita hivi vya dunia hii kwisha, tutakutana Naye mbinguni na kuwa na Ushirika tena; itakuwa Karamu ya Arusi. “Sitakunywa divai tena ama kula ya matunda, hata nitakapokula na kunywa pamoja nanyi upya katika Ufalme wa Baba Yangu.” Hiyo ni kweli?

¹⁰⁹ Tazama tena, Melkizedeki alikwenda kumlaki Ibrahimu kabla yeye hajarudi nyumbani. Tuna mfano mzuri jinsi gani hapa; Melkizedeki akimlaki Ibrahimu kabla hajafika nyumbani baada ya vita. Tutamlaki Yesu hewani kabla hatujafika nyumbani! Hiyo ni kweli. II Wathesalonike inatuambia hivyo, kuwa tutamlaki hewani. Mfano mzuri wa Rebeka akimlaki Isaka kondeni wakati wa jua kupunga. Tutamlaki hewani. II Wathesalonike inatuambia hivyo: “Kwa maana sisi tulio hai, tutakaosalia, hatutawatangulia ama kuwazuia, wao waliokwisha kulala mauti; kwa maana parapanda ya Mungu italia; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza; sisi tulio hai tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu kumlaki Bwana hewani.” Kamilifu! Mifano hii yote.

¹¹⁰ Kwa hivyo ule mwili wa kiungu, kama umekufa na kuingia kwenye mwili huo wa kiungu inakuwaje? Huo mwili wa kiungu unashuka ardhini kuchukua ule mwili uliokombolewa. Na iwapo umo humu hewani, unachukua mwili kuulaki ule mwili wa kiungu (ndivyo hivyo), na kunyakuliwa kwenda kumlaki Bwana hewani.

¹¹¹ Nani huyu Melkisedeki ila Mungu?

¹¹² Basi, tunaona hapa dhahiri siri yote ya safari yetu maishani, na mauti, na tunapokwenda baada ya mauti. Pia kuchaguliwa kimbele kunaonekana wazi hapa. Naam, sikiza tunapofundisha haya, kwa makini.

¹¹³ Zile hatua za—za kusudi Lake la milele alizokuwa nazo sirini sasa tayari zimefunuliwa. Tazama, kungali kuna hatua

tatu kufikia ukamilifu. Jinsi tu anavyoukomboa ulimwengu; vivyo hivyo hukomboa kanisa Lake. Yeye hukomboa watu katika hatua tatu. Sasa tazama, kwanza ni Kuhesabiwa Haki kama alivyohubiri Luther; pili, Kutakaswa kama alivyohuburi Wesley; tatu, Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli! Ndipo kunyakuliwa kunakuja.

¹¹⁴ Sasa, ulimwengu, Yeye alikomboaje ulimwengu? Alichofanya kwanza ulipotenda dhambi, aliusafisha kwa ubatizo wa maji. Hiyo ni kweli. Kisha akamwaga damu Yake juu Yake kutoka msalabani na kuutakasa na kuuita Wake Mwenyewe. Ndipo akafanyaje? Kama vile alivyourarua ulimwengu wote kotoka kwako na kufanya upya vitu vyote kwa ubatizo wa moto wa Roho Mtakatifu, Yeye pia ataufanya upya ulimwengu. Nao utauchomwa moto na kuondolea mbali kila viini kwa umbali wa maili milioni kadhaa kwenda juu, na kila kitu kitafagiliwa mbali. Na kisha kutakuweco mbingu mpya na nchi mpya, jinsi tu ulivyo kiumbe kipya katika Kristo Yesu Roho Mtakatifu anapokuja kwako. Unaona, ndivyo hivyo. Yote ni wazi iwezavyo kuwa.

¹¹⁵ Kila kitu kiko katika utatu. Kuzaliwa kwa kawaida kumo katika utatu. Jambo la kwanza linalotukia ni nini mwanamke anapopata mtoto? Nini hutoka kwanza Maji. Nini hufuata? Damu. Kinachofuata ni nini? Uhai. Maji, damu, Roho. Inakuwaje kwa mmea? Huoza. Kitu cha kwanza ni nini? Ubua, Kinachofuata? Kishada. Halafu? Kapi. Ndipo mbegu hutokea hapo. Hatua tatu tu zake hata inapofikia mbegu. Bila shaka.

¹¹⁶ Mungu huthibitisha hayo. Hiyo imekuwa kweli daima; Mungu hithibitisha kuwa kweli. Inaonyesha wazi wazi ya kwamba aliyechaguliwa kimbele ndiye tu anayefikiriwa katika ukombozi. Umeshika hilo. Hebu niseme tena. Yule aliyechaguliwa kimbele ndiye tu anayefikiriwa katika ukombozi. Watu huenda wakajifanya, wakadhani wamekombolewa bali ukombozi halisi ni kwa wale waliochaguliwa kimbele. Kwa maana neno komboa lenyewe maana yake ni “Kurudisha!” Hilo ni kweli? *Kukomboa* ni kitu... *Kukomboa* cho chote ni kukirudisha mahali pake pa asili. Haleluiya! Kwa hivyo ni wale walichaguliwa kimbele tu watakaorudishwa, kwa sababu wengine hawakutoka pale. Unaona? Kurudisha.

¹¹⁷ Kuwa wa milele pamoja Naye hapo mwanzo... Ule Uzima wa Milele uliokuwa nao, wazo Lake la ulivyokuwa, alitaka tu wewe—Alitaka mi—mi nisimame mimbarani, tuseme. Alikutaka wewe uketi kitini usiku wa leo. Ndipo tunatekeleza kusudi Lake la milele. Na yeye aliyeondoka nyumbani, alikuja tu ulimwenguni kutekeleza kusudi Lake. Sivyo? Naam. Ndipo inapokwisha, unarudishwa tena katika hali ya utukufu. Unakomaa na kurudishwa tena.

¹¹⁸ Si ajabu Paulo angesema walipokuwa wakijenga gogo la kukatia kichwa chake. Alisema, “U wapi, Ewe mauti, uchungu wako? Ku wapi, Ewe kaburi, kushinda kwako? Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye ushindi!” Akasema, “Mauti, niambie ambapo waweza kunifanya nikapiga mayowe. Kaburi, hebu niambie, utanishikiliaje, kwa sababu mimi nina Uzima wa Milele.” Amina! Yeye aliitambua. Mauti, kuzimu, kaburi, hamna kingelimshikilia. Na hamna kitu kinachoweza kutudhuru, tuna Uzima wa Milele. Alitambua ya kwamba amebarikiwa kwa Uzima wa Milele.

¹¹⁹ Kama tu tone la umande. Kama naelewa, ni... Sijui kemia sana, bali halina budi kuwa kuganda kwa unyevu ama hewa... Na usiku unapokuwa baridi na wenye giza, hilo huanguka kutoka mbinguni na kuanguka ardhini. Limeanguka kutoka mahali fulani. Bali asubuhi inayofuata kabla jua halijachomoza, limekaa pale, maskini tone hilo, likitetemeka, bali hebu jua lichomoze, tazama likimetameta. Lina furaha, kwani? Jua litaliita moja kwa moja kurudi lilikotoka. Na vivyo hivyo Mkristo. Haleluya. Tunajua tunapoenda uweponi mwa Mungu, kitu fulani ndani yetu kinatuambia ya kwamba tumetoka mahali fulani na tutarudi tena kwa zile nguvu ambazo zinatuvuta.

¹²⁰ Tone hilo la umande humetameta na kuangaza na kupaza sauti, kwa sababu linajua limetoka kule juu na lile jua litaliinua juu kule tena. Na mtu ambaye ni sifa ya Mungu, aliyezaliwa na Mungu anajua (Halleluya!), anapompata Mwana wa Mungu, atainuliwa atoke hapa siku moja! “Kwa maana Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote Kwangu.” Amina!

¹²¹ Sasa tazama! Sasa tunaona Melkizedeki na kwa nini Mariamu hakuwa mama Yake. Hiyo ndiyo sababu Yeye alimwita mwanamke, sio mama. Hana baba, kwa kuwa alikuwa Baba, baba wa milele, wale watatu katika mmoja. Hana mama, bila shaka. Hana baba, kwa kuwa Yeye alikuwa Baba. Kama mshairi alivyonena sifa za Yesu. Akasema,

MIMI NDIYE niliyenena na Musa
Kwenye kijiti kilichowaka moto.
MIMI NDIYE Mungu wa Ibrahimu,
Ile nyota yenye kungaa ya asubuhi.
Mimi ni Alfa, Omega, mwanzo kutoka
mwisho.
Mimi ni uumbaji wote,

Na Yesu ndilo hilo Jina. (Hiyo ni kweli!)

Jamani, mnasema mimi ni nani?
Wao husema nilitoka wapi?
Je, mnajua Baba Yangu,
Au je, mnaweza kusema Jina lake? (Halleluya!)

¹²² Hilo ndilo Jina la Baba. “Naam, Nimekuja katika Jina la Baba Yangu na hamkunipokea.” Waona? Hakika. Yeye ni yeye yule jana leo, na hata milele.

¹²³ Naye huyu Melkizedeki akafanyika mwili. Yeye alijifunua mwenyewe kama Mwana wa Adamu alipokuja kama nabii! Alikuwa katika majina matatu ya Mwana, Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, Mwana wa Daudi.

¹²⁴ Alipokuwa hapa duniani alikuwa mwanadumu kutimiza Maandiko. Musa alisema, “Bwana Mungu wenu atakuondokeshea nabii kama nilivyo mimi.” Kwa hivyo ilimpasa kuja kama Nabii. Hakusema kamwe, “Mimi ni Mwana wa Mungu.” Alisema, “Mimi ni Mwana wa Adamu. Unaamini Mwana wa Adamu?” Bila shaka hiyo ndiyo ilimpasa kushuhudia, kwa sababu hivyo ndivyo alivyokuwa. Sasa amekuwa katika Jina lingine la Mwana, Mwana wa Mungu, asiyeonekana, yule Roho. Na ajapo tena, ni Mwana wa Daudi kusudi aketi kwenye Kiti Chake cha Enzi.

¹²⁵ Basi, alipokuwa hapa na akafanyika mwili, aliitwa Mwana wa Adamu. Sasa, alijitambulishaje kwa ulimwengu kama Mwana wa Adamu, yule nabii?

¹²⁶ Siku moja nilikuwa nikisimulia hadithi ya Petro na Andrea nduguye. Walikuwa wavuvi, naye baba yao Yona alikuwa mzee mwamini mkuu. Siku moja walisema aliketi kando ya mtumbwi. Akasema, “Mwanangu, unajua jinsi tulivyoomba tulipohitaji samaki.” (Wao walikuwa wafanyi biashara ya uvuvi) Akasema, “Tulimtumainia Mungu, Yehova, kwa riziki. Nami nazeeka sasa; sitaweza kukaa nanyi wavulana muda mwingi zaidi. Nami daima—pamoja na waumini wote wa kweli—tumetazamia wakati wa kuja kwa masihi. Tumekuwa na wa aina zote wa bandia, bali siku moja wa kweli atakuja.” Naye akasema, “Masihi huyu ajapo, siwataki enyi wavulana mkadanganyike. Huyu Masihi hatakuwa tu mwanatheologia, Yeye atakuwa nabii. Kwa mana nabii wetu Musa, tunayemfuata, alisema. . .” Sasa Myahudi ye yote ataamini nabii wake. Amefuzwa kujua hilo. Na na—nabii akisema cho chote ambacho ni kweli, basi hiyo ni kweli. Bali Mungu alisema, “Kukizuka katikati yako mtu wa rohani ama nabii, Mimi Bwana nitajifunua kwake. Na asemayo yakitimia, ndipo msikizeni na kumwogopa. Bali kama hayatimii, basi msimwogope kamwe.” Mwaona? Kwa hivyo hilo ndilo lilokuwa thibitisho la nabii.

¹²⁷ “Kwa hivyo Musa alikuwa nabii aliyethibitishwa kweli kweli, na akasema, ‘Bwana Mungu wenu atakuondokeshea, miongoni mwa ndugu zenu, nabii kama nilivyo mimi. Na wote wasiomsikiza watatengwa na watu.’” Akasema, “Sasa watoto, kumbukeni, sisi Waebrania tunaamini manabii wa Mungu waliothibitishwa.” Sasa sikizeni kwa makini, msilikose. Na akasema, “Masihi ajapo, mtamjua, kwa maana atakuwa nabii

Masihi. Naam, nilisema, imekuwa miaka mia nne; hatujapata nabii tangu Malaki. Bali atakuwa!”

¹²⁸ Siku moja baada ya kifo chake, miaka michache, mwanaye Andrea alikuwa akitembea ukingoni, naye akasikia mtu wa porini kutoka jangwani akisema, “Huyo Masihi amesimama miongoni mwenu sasa.” Tai huyo mkubwa aliyeinuka nyikani na kupuruka pale, kasema, “Masihi yumo miongoni mwenu hivi sasa. Hatumjui bado, bali anasimama miongoni mwenu. Nitamjua, kwa sababu nitaona ishara ikitoka Mbinguni.” Siku moja akasema, “Pale, tazama, Mwana-kondoo wa mungu azichukua ye adhambi za ulimwengu.”

Akaondoka akaenda—akaenda, mtu huyu, kumtafuta ndugu yake; akasema, “Simoni, nataka uje humu; tumempata Masihi.”

“Nenda huko Andrea unafahamu vema zaidi ya hayo!”

“Naam, najua lakini yule—mtu huyu ni tofauti.”

“Yuko wapi? Ametoka wapi?”

“Yesu wa Nazarethi.”

“Maskini mji huo muovu? Naam, hangekuja kutoka mji muovu, mchafu kama huo.”

“Njoo tu uone.”

¹²⁹ Mwishowe akamshawishi kwenda huko chini siku moja. Basi alipokuja mbele ya Masihi huyu, Yesu, akisimama pale akinene na watu. Alipoenda mbele Zake, Yeye alisema, “Jina lako ni Simoni na u mwana wa Yona.” Hiyo ilitosha! Akapata funguo za Ufalme! Kwa nini? Alijua ya kwamba mtu huyo hakumjua. Naye alimjuaje na yule baba mzee mcha mungu aliyemfundisha jinsi ya kuamini Masihi?

¹³⁰ Kulikuwa mtu aliyekuwa amesimama pale jina lake Filippo. Lo, aliamshwa sana! Alimjua mtu mwingine waliyesoma Biblia pamoja naye. Naye akazunguka kilima kile, na akampata pale kwenye mizeituni yake. Alikuwa ameinama chini, akiomba. Walikuwa tayari wamepata mafundisho mengi ya Biblia pamoja. Ndipo akatokea nje pale, na akasema, baada ya kumaliza maombi, akasema, “Njoo uone tuliyempata, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu. Yeye ndiye masihi tunayemtazamia.”

Sasa, naweza kumsikia Nathanieli akisema, “Nini, Filippo, nakusudia hujatumbukia kilindini, sivyo?”

¹³¹ “La, hashu! Sivyo. Naam, hebu nikueleze. Wajua, tumesoma Biblia pamoja, na je, nabii alisema masihi atakuwa nini? “Atakuwa nabii. Je, unakumbuka yule mzee mvuvi uliyenunua samaki kwake, ambaye hakuwa na elimu angaa ya kuandika jina lake, aliyeitwa Simoni?”

“Naam, ah, ah!”

¹³² “Alikuwa, na wajua nini? Huyu Yesu wa Nazareti akamwambia jina lake lilikuwa Simoni, akageuza jina lake

likawa Petro, maaana yake “jiwe dogo,” na kumwambia babake alikuwa nani.”

Naam, akasema—akasema, “Sijui, laweza nano jema kutoka Nazareti?”

¹³³ Akasema, “Hebu tusizungumze habari hiyo; njoo tu uone.” Hilo ni wazo jema. Njoo uone. Kwa hivyo yuaja Filipo akimleta Nathanieli. Alipofika—Yesu huenda alikuwa amesimama akihubiri, labda akiombea wagojwa kwenye mstari wa maombi—na alipofika alipokuwa Yesu, Yesu akamgeukia na kusema, “Tazama, Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake.”

¹³⁴ Naam, mnasema, “Ni kwa sababu ya nguo alizovaa.” Sivyo hasa! Watu wote wa mashariki huvalia sawa. Angalikuwa Mshamu ama ye yote yule, ndevu, vazi.

¹³⁵ Akasema, “Tazama Mwisraeli kweli, kweli, hamna hila ndani yake.” Kwa maneno mengine, mtu mwaminifu na mnyenyekevu. Vema, hilo lilimtoa pumzi Nathanieli. Naye akasema, “Rabi (maana yake “mwalimu”) Rabi, ulinijua lini? Ulijuaje nilikuwa Myahudi? Ulijuaje ni mwaminifu, sina hila?”

¹³⁶ Akamwambia, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya ule mti, nilikuona.” Umbali wa maili kumi na tano, ng’ambo ya nchi hiyo siku iliyotangulia. Yeye alisemaje? “Rabi, wewe u mwana wa Mungu. Ndiwe mfalme wa Israeli!”

¹³⁷ Bali kulikuwako wale makuhani, wenye kiburi, wagumu, kasema, “Mtu huyu ni Belzebuli, mpiga rami.”

¹³⁸ Yesu akasema, “Nitawasamehe hilo...” Sasa kumbuka, hawakusema hayo kwa sauti kubwa kamwe, bali walisema hayo mioyoni mwao. Naye akatambua mawazo yao, Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo Biblia isemavyo. Liite kushirikiana mawazo ukitaka, bali Yeye—Yeye alijua mawazo yao.

¹³⁹ Naye akasema, “Nawasamehe hilo, lakini siku moja Roho Mtakatifu atakuja na kutenda jambo lile lile (baada ya kuondoka Kwake); kunena neno moja dhidi Yake, haitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu au ulimwengu ujao.” Sivyo? Sasa, hao walikuwa Wayahudi.

¹⁴⁰ Ndipo siku moja alitaka kwenda Samaria. Bali kabla hatujafanya hivyo, tuna yule mwanamke, au yule—yule mwanamume baada ya kupita mlango ulioitwa “Mzuri”, kwamba aliponywa, naye Yesu alijua hali yake, na akamwambia, “Chukua kitanda chako uende nyumbani.” Naye akafanya hivyo na kapata nafuu. Ndipo tunaona wale Wayahudi, wengine wao walimpokea; wengine wao walimwamini; wengine hawakuamini. Kwa nini hawakuamini? Wao hawakuchaguliwa Uzima... Hawakuwa sehemu ya zile sifa.

¹⁴¹ Sasa kumbukeni, wale walikuwa makuhani na watu mashuhuri. Naye Yesu... Wazieni kuhusu wale wanatheologia na makuhani, watu ambao haungalipata waa lo lote maishani

mwao. Yesu alisema, “Ninyi ni wa baba yenu ibilisi, na kazi zake mnatenda.” Kasema, mngalikuwa wa Mungu mngaliniamini mimi. Msiponiamini mimi, aminini—aminini kazi ninazotenda; zinashuhudia mimi ni nani.

¹⁴² Basi, Biblia ilisema kwamba Yesu ni yeye yule jana, leo na hata milele. Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi yeye aniaminiye mimi atazifanya pia.” Sivyoy? Tazama, huyo alikuwa Melkizedeki halisi sasa.

¹⁴³ Tazama tena. Kulikuwako na mataifa matatu tu ya watu. Mmenisikia mimi nikisema, nilikuwa mtenganishaji. Ndivyo. Wakristo wote ni watenganishaji, si watenganishaji wa rangi, bali watenganishaji wa roho. Rangi ya mtu haifai kitu. Yeye ni mwana wa Mungu kwa kuzaliwa. Bali Mkristo, Mungu alisema, “Jitengani, tokeni kati yao, na kadhalika.” Yeye ni mtenganishaji wa uchafu, kati ya kweli na Uongo.

¹⁴⁴ Bali tazama, walikuwa na ubaguzi wakati huo, ubaguzi wa rangi, ambao ni Wasamalia. Kuna mataifa matatu tu ya watu duniani, iwapo tunaamini Biblia; hao ni watu wa Hamu, Shemu na Yafethi. Hao ni wale wana watatu wa Nuhu. Sote tulitoka hapo. Naam. Hiyo inaturudisha sote kwa Adamu, ambayo inatufanya sote ndugu. Biblia ilisema, “Kwa damu moja Mungu aliumba mataifa yote.” Sote ni ndugu kwa damu ile. Mtu mweusi anaweza kumpa mzungu damu na kadhalika. Mzungu anaweza kumpa M—Mjapani, mtu majano, au Muhindi, mtu mwekundu, au ye yote yule, au . . . ? ama ye yote yule. Angeweza kumpa damu, kwa kuwa sote tuna damu moja. Rangi ya ngozi yetu, tunakoishi, haifai kitu. Bali tunapotenganishwa ndipo tunapotoka ulimwenguni, kama alivyowapandisha Waisraeli kutoka Misri. Hapo ndipo tunapotenganishwa na mambo ya ulimwengu.

¹⁴⁵ Sasa, kulikuwako “Watu wa Hamu, Shemu na Yafethi.” Na kama tunaweza kufuatilia vizazi kule nyuma, tungeona Wa-Anglo-Saxon, kule walikotoka. Basi hao walikuwa Wayahudi, Wasamaria, ambao walikuwa nusu Wayahudi na Mataifa, waliooana na Mataifa kwa ujanja wa Baalamu, na Wamoabu. Walikuwa Wasamaria, na kulikuwa Wayahudi na Mataifa. Sasa, sisi Wa-Anglo-Saxon hatukuhusika; hatukuamini Masihi ye yote, ama cho chote kile. Hatukutarajia ye yote. Tuliingizwa baadaye. Yesu alikuja Kwake, nao walio Wake hawakumpokea. Basi akawaambia wanafunzi Wake. “Katika njia ya mataifa msiende, afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.” Naye akawaendea tu kondoo waliopotea wa Israeli. Na tazama, yeye alijidhihirisha Mwenyewe kama Mwana wa Adamu mbele za Wayahundi. Wakamkataa. Basi, Wasamaria, ambao ni nusu Wayahundi na nusu Mataifa, waliaamini pia na walikuwa wakimtazamia Masihi. Hatukumtazamia; tulikuwa makafiri wenye rungu mgongoni, wenye kuabudu sanamu, mataifa.

¹⁴⁶ Bali sasa siku moja (Mt. Yohana 4) alikuwa hana budi kupitia Samaria akielekea Yeriko. Bali ali—akazunguka Samaria. Na alipokuwa akienda kule akaketi kwenye kisima nje ya mji uitwao Sikari. Na kisima kile, iwapo umewahi kuwa pale, ni mahali padogo panapovutia kama hapa hivi, na mna chemichemi ya umma pale, maji ambapo walikuja wote. Na wanawake huja asubuhi, wakachota nyungu za maji wakaziweka vichwani mwao, na moja kwenye kila kiweo, na kutembea wima iwezekanavyo, bila kumwaga hata tone, huku wakizungumzana. Kwa hivyo wao—wale watu huja kule.

¹⁴⁷ Kwa hivyo hii ilikuwa yapata saa 5:00 mchana. Kwa hivyo akawatuma wanafunzi Wake mjini kununua mlo, chakula. Na walipokwisha kuondoka, akaja mwanamke mwenye sifa mbaya; tungemwita leo “mwanake nuru nyekundu” ama malaya; alikuwa na waume wengi zaidi.

¹⁴⁸ Kwa hivyo Yesu alipokuwa ameketi pale, huyu mwanamke akaja kama saa tano hivi. Unaona, yeye hangaliambatana na mabikira walipokuja asubuhi kuchota maji ya kuoga; ilimpasa kungojea hata wote... Hawakuchanganyikana kama wafanyavyo leo. Alikuwa ametiwa alama. Kwa hivyo akaja kuteka maji. Hivyo basi akatwaa tu ile winchi ya kale, akatia chango kwenye balasi na akaaza kuishusha; akasikia mtu akisema, “Mama, niletee maji” Sasa, kumbuka, huyu ni Melkizedeki; huyu ni Yesu jana, Mwana wa Adamu.

¹⁴⁹ Naye akageuka, akaona Myahudi. Ndipo akasema, “Bwana, haifai Myahudi kumuomba Msamaria cho chote. Mimi ni mwanamke Msamaria, kwa hivyo umekosea. Haikukupasa kuniomba kitu kama hicho; hatuchangamani.”

¹⁵⁰ Akasema, “Bali kama ungaliujua ni Nani anayezungumza nawe, ungalinionamba mimi maji.” Akasema, “Utayatekaje. Kisima ni kirefu, na huna kitu cha kutekea.”

¹⁵¹ Yeye akasema, “Maji niyatoayo ni maji ya Uzima yanayobubujikia Uzima wa Milele.” Akanena naye hata akajua hali yake ilivyokuwa. Ndipo akamwambia—tazama alivyomwambia sasa. “Nenda kamwite muneo, uje naye hapa.” Naye akasema, “Sina mume.”

¹⁵² Akasema, “Umesema vema, kwa maana umekuwa na waume watano, naye uliye naye sasa siye mume wako; hapo umesema kweli.” Tazama tofauti ya mwanamke huyo na kile kikundi cha makuhani. Alimjua Mungu zaidi kuliko lile kundi lote la makuhani pamoja.

¹⁵³ Akasema, “Bwana, naona ya kuwa wewe ni nabii!” Akasema, “Hatujapata mmoja kwa muda wa miaka mia nne. Sasa, tunajua ya kwamba Masihi yu aja, naye atakapokuja hivyo ndivyo atakavyotenda.” Hiyo ilikuwa ishara ya Masihi, kwa kuwa alikuwa Mwana wa Adamu. Kasema, “Hivyo ndivyo atakavyotenda ajapo, huna budi kuwa nabii Wake.”

¹⁵⁴ Naye akasema, “Mimi ndiye.” Hapana mwingine angalisema hayo!

¹⁵⁵ Akaangusha ule mtungi wa maji, na kukimbia mjini, na kusema, “Njoooni, mtazame mtu aliyeniambia niliyotenda. Je, haiyamkini huyu siye yule Masihi?” Sasa kumbukeni, Yeye aliahidi kutenda jambo lilo hilo mwishoni mwa jamii ya mataifa. Wayahudi tayari walikwisha kuwa na miaka elfu nne kumtarajia huyo Masihi, miaka elfu nne wakifundisha Yeye yuaja, na atakayotenda afikapo kule; nao wakashindwa kumwona, wakashindwa kumtambua. Naye alipojitambulisha kwa masharti yale yale ya Biblia aliyosema angejitambulisha kwayo, huku akiwa tayari amekwisha kufanyika ule mwili wa kiungu na kisha akafanyika mwili na kukaa kwao, wakashindwa kuiona, na kuziita kazi Zake kazi za ibilisi.

¹⁵⁶ Naam, tumekwisha kuwa na miaka elfu mbili ya mafundisho, yakipitia kwa kanisa Katoliki la Kirumi, baada ya wale mitume. Ndipo yakapitia kwa Katoliki ya Kirumi, Wayunani, na kadhalika, hata kwa wakati wa Luther, na Wesley, wo wote wale, madhehebu mia tisa bali mbali. Kote kote, walikuwa wakifundisha katika nyakati hizi zote. Sasa, Yeye aliahidi kwamba kabla tu ule wakati wa mwisho haujawadia ile picha ya Sodoma na Gomora tena ita... Kama ilivyokuwa siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa wakati wa mwisho ujapo, Mwana wa Adamu atajifunua tena.” [Mahali pa tupu kwenye kanda—Mh.] “Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa mimi—(Neno la kumtaja mtu),—nitakuwa pamoja nayi, hata ndani yenu, hata itimilivu, mwisho wa dahari. Nitakuwa pamoja nanyi.” Ni yeye yule jana leo na hata milele.

¹⁵⁷ Mnaona—mnaona yule Msamaria hasa alikuwa—kutoka mahubiri yangu ya usiku uliopita—alikuwa Hagai (mnaona?) kitu kilichopotoshwa. Wayahudi walikuwa Sara—au Wasara; bali mataifa ni wa Miriamu, Uzao wa Kifalme. Uzao wa kifalme wa Ibrahimu.

¹⁵⁸ Sasa, imeahidiwa ya kwamba katika hizi siku za mwisho ya kwamba Mungu yule yule, Kristo yule yule, angerudi na kujifunua Mwenyewe kama Mwana wa Adamu. Kwa nini? Ni yeye yule jana, leo na hata milele. Na kama aliwaachilia wale Wayahudi wapuuze hayo—na kuwaonyesha ile ishara ya Masihi, na ndipo aje kwenye mwisho wa mafundisho ya mataifa na kuwaachilia waendeleo kwa theologia, Yeye angekuwa asiye haki. Inampasa atende jambo lile lile, kwa kuwa Biblia ilisema, katika 13—Waebrania 13:8, Yeye ni yeye yule. Naye aliahidi katika Malaki 4 na yale Maandiko yote mbali mbali ya kwamba kwenye siku za mwisho kanisa lingekuwa hasa kama lilivyo siku hizi na ulimwengu pia.

159 Tazama ulimwengu siku hizi. Tazama ile hali ya Sodoma. Tazama matetemeko ya nchi mahali mahali na mambo yanayotukia. Tazama kanisa katika machafuko lililomo, ya Babeli. Tazama wajumbe wake, Oral Roberts fulani na Billy Graham fulani. . . *G-r-a-h-a-m*. Mara ya kwanza kabisa ambapo tumepata mjumbe kwa makanisa yote ambaye jina lake linaishia hasa kwa *h-a-m* kama Abraham. *A-b-r-a-h-a-m* ni herufi saba-*G-r-a-h-a-m* ni herufu sita. Yuko wapi? kwa ulimwengu. Sita ni namba ya mwanadamu. Mwanadamu aliumbwa siku ya sita. Bali saba ni namba ya Mungu.

160 Basi, watazame kule chini Sodoma. Nao wajumbe wao wamo kule wakiwahubiria. Bali je, Uzao wa kifalme wa Ibrahimu uko wapi? Je, ishara yao iko wapi, ambayo yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” ambapo Mungu alishuka na akadhirishwa katika mwili wa mwanadamu, na akasema yale Sara aliyokuwa akifikiria moyoni mwake hemani nyuma yake, ile ishara ya mwisho kabla ulimwengu wa Mataifa haujaangamizwa kwa moto? Nalo kanisa tayari limeonyeshwa ishara yake ya mwisho kabla ulimwengu wote haujaangamizwa, ufalme huu wa Mataifa utaangamizwa kwa moto na ghadhabu ya Mungu. Je, mnaamini hayo?

161 Yule Melkizedeki alikuwa mwili, alijiwakilisha katika mwili wa binadamu; na ndipo baadaye akafanyika mwili. Na sasa usiku wa leo, Yeye ni yeye yule jana leo na hata milele. Je, mnaamini hayo?

162 Je, huyu Melkizedeki basi ni nani, ambaye ni yeye yule jana. . . Hana baba, hana mama, hana mwanzo wa siku Zake kamwe, Yeye hana mwisho wa uhai Wake. Naye alikutana na Ibrahimu, Naye alifanya ishara gani? Ndipo alipofanyika mwili, Yeye alisema itajirudia tena kabla ule mwisho haujaja. Je, mnaamini hilo? Naamini! Hebu na tuombeni.

163 Mungu mpendwa, naamini Maandiko, ambapo umesema ni Wewe yule jana, leo, na hata milele. Na kwa unyenyekevu sana moyoni mwangu, Bwana, najua ya kwamba jambo fulani karibu litukie. Siwezi kulitambua vizuri: naogopa kusema cho chote Bwana. Wewe unajua moyo wa mtumishi Wako.

164 Na ni mara ngapi kote kote kwenye zile nyakati ulipotuma vitu, watu wakashindwa kuvitambua. Mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa yale Yeye aliyotenda, na kusema jinsi atatenda mambo makuu siku za usoni, bali anapuuza yale Yeye anayotenda sasa. Imekuwa vivyo hivyo nyakati zote. Mbona kanisa la kirumi likashindwa kumtambua Mt. Patrick kama nabii wa Mungu? Mbona wakamuua Joan wa Ark naye alikuwa na—nabii mwanamke, wakamchoma kama mchawi? Baba kila mara ni yaliopita, umeyaficha wenye hekima na akili. Si ajabu uliwaambia wale makuhani, “Mwajenga makaburi ya manabii, nanyi ndio miliowaweka mle ndani.” Baada yao kuondoka, ndipo

wao huona makosa yao. Wao kila mara hukutesa Wewe, Bwana, katika hali yo yote unayokuja.

¹⁶⁵ Naomba usiku wa leo, Mungu, mara hii tu. Kesho tunapaswa kuwa—kuwa Tucson. Sehemu zingine ulimwenguni, inatupasa kuhubiri katika miji mingine. Lakini Mungu mpendwa, huenda ikawa kuna wageni hapa usiku wa leo ambao bado hawaja—wamesikia maneno yakihubiriwa, bali hawajaona yakidhihirishwa. Kama nilivyokuuliza hapo mwanzo... Wale wanafunzi, Kleopa na rafiki yake walipokuwa wakija kutoka Emau walikuwa wakienda njiani. Nawe ukatoka kichakani na kuanza kuzungumza nao baada ya kule kufufuka, ukawahubiria... Naam, akasema, “Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito, je! hamjui kwamba ilimpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu Wake?” Bali hata hivyo hawakuitambua. Siku nzima walitembea Nawe na hata hivyo hawakukujua. Bali usiku mmoja... Usiku ukaingia, wakakushawishi kuingia. Walipoingia katika chumba kile kidogo na wakafunga milango yote, ndipo ukafanya jambo fulani jinsi ulivyofanya kabla ya kuangikwa Kwako: nao wakatambua ilikuwa Kristo aliyefufuka. Mara ukaingia nyuma ya lile pazia na kutoweka. Wakaondoka haraka na kuwaambia wale mitume, “Bwana amefufuka kweli kweli!”

¹⁶⁶ Baba Mungu, naamini Wewe ungali hai. Najua ungali hai. Nawe umetuthibitishia mara nyingi sana. Je, ungeweza kufanya hivyo mara hii tu kwetu, Bwana? Iwapo tulipata neema mbele Zako, hebu na itendeke mara nyingine. Mimi ni mtumishi Wako, hawa ni watumishi Wako humu ndani. Bwana, yote ambayo nimesema hayange... Neno moja tu kutoka Kwako lingekuwa zaidi ya yale nimesema katika siku hizi tano ama jumbe tano. Ingekuwa zaidi, neno moja kutoka Kwako. Je, mbona usinene, Bwana, watu wapate kujua ya kwamba nimewaambia yaliyo kweli. Tujalie, Mungu. Naomba katika Jina la Yesu mara hii tena. Amina.

¹⁶⁷ Sasa, sikujui wewe, nawajua watu wengine. Najua kijana huyu anayeketi hapa. Namjua Bill Dauch anayeketi pale. Nataka ku... Hapa yupo Ndugu Blait, Rodney Cox. Ni vigumu kuona kule. Upande huu wakati huu siwezi kuona mtu ninayemjua hasa.

¹⁶⁸ Sasa, ni wangapi humu wanaojua kwamba mimi ni mgeni kwenu, inueni mikono yenu, wanaojua sijui cho chote juu yao, inueni mikono yenu pande zote mbili. Wangapi hapa wana kasoro fulani ama jambo ambalo—ambalo mnajua sijui cho chote kulihusu, tafadhali inueni mikono yenu. Sasa, haingeliwezekana kabisa, hata kidogo, haiwezekani kamwe kwangu kujua lo lote kukuhusu. Kama sivyo, basi haina budi kuja kwa ufunuo wa Roho. Na kama nimewaambieni siku hizi zote, na usiku wa leo yeye si mfu, Yeye yuko hapa na aliahidi kutenda jambo lile lile, na akaahidi ya kwamba kungekuja wakati siku za mwisho

kulingana na Malaki 4 na kulingana na Mt. Luka, ya kwamba Yeye angeonekana tena katika mwili wa binadamu miongoni mwa watu Wake, na kutenda mambo yale yale, na kufunua mambo yale yale, ishara ile ile ya Kimasihi. . . Je, ni wangapi wanaojua hivyo enyi wasomaji wa Biblia—wanaojua hiyo, ni kweli waseme, “Amina”. [Makutano wanaitikia, “Amina!”—Mh.] Hapana budi nyote ni wasomaji wa Biblia.

¹⁶⁹ Sasa, najua ni jambo la kigeni kwa watu leo, bali ni kweli. Hiyo ndiyo sababu hawakumjua Yesu wa Nazareti. Walijua kanuni za imani za makanisa yao, lakini hawakumjua Yeye. Bali alikuja tu vile Biblia ilivyosema, si kama mwanatheologia au kuhani; Yeye alikuja kama Nabii; na walio Wake hawakumpokea.

¹⁷⁰ Sasa, ikiwa Mungu atadumisha Neno Lake, na ikiwa nita—itatukia na kumjia mtu fulani nimjuaye, basi nita—nitampata mtu mwingine. Mnaona, namtaka mtu fulani nisiyemjua. Na nawatakeni muombe.

¹⁷¹ Sasa tazameni, wakati mmoja palikuwa na mwanamke maskini mwenye udhaifu. Alitumia pesa zake kwa madaktari; na hawakumsaidia chochote. Na alisema moyoni mwake, “ikiwa nitagusa tu vazi la Mtu yule, nitakuwa mzima.” Je, mnakumbuka hadithi hiyo? Kwa hivyo wote wakajaribu kumrudisha nyuma, bali alijikasa hata akaligusa vazi Lake, akarudi nyuma na kuketi chini.

¹⁷² Sasa, sikizeni kwa makini. Basi Yeye alipofanya hivyo—mwanamke yule alipofanya hivyo, Yesu akageuka na kusema, “Nani alinigusa Mimi?”

¹⁷³ Naam, mtume Petro alimkemea Yeye. Huenda alisema jambo kama, “Bwana usiseme jambo la namna hiyo. Watu wataamini una kasoro fulani, kwa sababu Wewe unawauliza wale nyama Zako na kunywa damu Yako. Tayari wao wanafikiri kuna kitu kilicho kasoro. Na sasa Wewe wasema, ‘Nani aliyenigusa Mimi,’ naam, makutano wote wanakugusa Wewe.”

¹⁷⁴ Akasema, “Naam, lakini naona ya kuwa nguvu zimenitoka! Huku kulikuwa kuguswa tofauti. Kila mtu anajua kwamba nguvu ni uweza. “Nimekuwa hafifu; nguvu zilinitoka, “Naye akageukia wale makutano hata alipomwona maskini mwanamke yule na kumwambia juu ya kutokwa kwake kwa damu. Naye akasikia mwilini mwake ya kwamba kutoka damu kwake kulikoma. Sivyo? Naye akasema, “Imani yako imekuokoa.” Naam, neno la Kiyunani ni *Sozo*, ambalo bila shaka maana yake ni “kuokolewa kimwili ama kiroho.” Vile vile, kuokolewa. Yeye ni—Yeye ni Mwokozi wako.

¹⁷⁵ Basi, iwapo huyo alikuwa yeye jana, na alivyotenda kuthibitisha kwamba alikuwa miongoni mwa watu Wake, Masihi aliyeahidiwa, na hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe

katika ahadi kwa Biblia, Yeye angetenda vile vile sasa. Je—je, Yeye si angepaswa kutenda jambo lile lile?

¹⁷⁶ Unasema, “Je, Yeye alisema ni kuhusu kuponya wagojwa?” Naam, Wabrana, Biblia ambayo nimeisoma hivi sasa ilisema Yesu Kristo sasa ndiye Kuhani wetu Mkuu ambaye anaweza kuchukuliana nasi katika mambo yetu ya udhaifu. Ni wangapi wanajua hilo ni kweli? Biblia ilisema hivyo. Yeye ni Kuhani Mkuu ambaye anaweza kuchukuliana nasi katika mambo yetu ya udhaifu. Basi iwapo ndiye Kuhani Mkuu yule yule ambaye alikuwa wakati huo, Yeye angetendaje sasa? Ingempasa kutenda vile vile alivyofanya wakati huo, iwapo Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule. Sasa, huenda uka... mimi si Kuhani Mkuu wenu. Huenda ukanigusa, na ingekuwa tu kama kumgusa mume wako, au ndugu yako, ama yeyote yule, mwanamume. Bali hebu na imani yako inguse Yeye na uone yatakayotendeka.

¹⁷⁷ Naam, kama mimi ni mtumishi wa Mungu na nimewaambia kweli, Mungu atadhihirisha hayo kuwa kweli. Na hiyo ingethihirisha ya kwamba Yesu Kristo yu aishi usiku wa leo, amesimama hapa. Hiyo ni kweli? Sasa iweni na imani upande mmoja kwa wakati mmoja, upande mmoja. Ninyi iweni na imani kule nje. (Afadhali nikae kwenye maikrofoni kwa sababu hawawezi kunisikia.)

¹⁷⁸ Mtu fulani na atazame juu kwa Mungu, na kusema, “Mungu, mtu huyo hanihui. Hajui cho chote kunihusu. Mimi ni mgeni kabisa kwake. Bali hebu na imani yangu ikuguse Wewe, Bwana. Na wajua kasoro yangu, Bwana. Unajua yote kunihusu; wewe unajua mimi ni nani, jinsi ulivyojua Petro alikuwa nani na kama ulivyomjua Nathanieli, na jinsi ulivyojua kilichokuwa kibaya kwa yule mwanamke mwenye kutokwa na damu. Na mtu huyu aniambia ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Basi, Bwana, hebu na imani yangu ikuguse Wewe.” Na kama Yeye atafanya hivyo na kujithibitisha bila kukosea hapa, ni wangapi wenu watamwamini kwa mioyo yenu yote, kama akimfanya angaa mmoja, ama wawili, ama watu watatu kwa—kwa ushuhuda! Mungu awabariki.

¹⁷⁹ Sasa, Baba Mungu, hii sasa haimo mikononi mwa mwanadamu kamwe; haina budi iwe ni tokeo la kimbinguni. Kwa hivyo naomba utanisaidia sasa, Bwana; mimi nimo mikononi Mwako. Tenda nami jinsi upendavyo. Katika jina la Yesu. Amina.

¹⁸⁰ Usiwe na wasiwasi, sema tu kwa unyenyekevu, na upole, “Bwana, nitakutumikia! Na hiyo itakuwa kweli ambayo... Kama ningaligusa vazi Lako basi nena kupitia kwa mtu yule. Hiyo itanithibitishia ya kwamba aliyosema ni kweli.” Hiyo ni kweli?

¹⁸¹ Je, ni wangapi wameshaona ile picha ya ile Nuru? Imeenea nchini, kila mahali. Sayansi imeichukua na kuichunguza na

kila mahali. Naam, Yeye yumo papa hapa, Yeye Yule aliyenena kuhusu Ndoa na Talaka [LILE NENO LILILONENWA, Kit. 3 Nam. 13—Mh.] Yeye yule yule aliyekuwa mlimani na kutikisa vilima nyuma kule, Yeye yule yule aliyekuwa chini huku mtoni mwaka wa 33, Yeye yule jana, leo na hata milele. Ni yeye yule.

¹⁸² Sasa, yuko mwanamke; naye anatambua sasa ya kwamba jambo fulani linatendeka. Nuru ile inanig'nia juu yake hasa. Anaketi papa hapa, yeye. . . Ana sweta kijani kibichi ama cho chote kile. Simjui huyu mwanamke. Nakisia sisi ni wageni. Hiyo ni kweli. Je, unaamini ya kwamba Mungu. . . Unahitaji kitu fulani, nawe je, unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia shida yako ni nini? Na akifanya hivyo, ndipo unajua haina budi kuwa uweza wa kimbinguni, kwa maana mimi sikujui. Nayo haina budi kufanyika kimbinguni. Inategemea unafikiri ni nini. Unaweza kuungana pamoja na wale makuhani, ukaiite ibilisi, au unaweza ukaungane na waaminio ukaiite Mungu. Cho chote unachoamini, hapo ndipo thawabu yako itatoka.

¹⁸³ Iwapo Mungu atanifunulia mimi shida yako, je, utamkubali kama—kama upatanisho wako kwa shida hiyo? Sijui shida hiyo ni nini, bali mimi najua na wewe unajua ya kwamba jambo fulani linaendelea.

¹⁸⁴ Naam, hebu nikuambie unavyojisikia, ndipo utajua, kujisikia kwema sana, kwa kupendeza, na kuburudisha. Naitazama hiyo moja kwa moja sasa. Ni ile Nuru, Nuru ya manjano inayoni'nia kutoka kwa huyu mwanamke. Naye bibi huyu ana shida tumboni mwake. Ni kitu kama kivimbe tumboni mwake. Yeye hatoki hapa, la; umetoka mbali na hapa, sivyo? Hiyo ni kweli! Umetoka Winsconson. Sivyo? Bila shaka. Sasa, umeponywa. Imani yako imekuponya.

¹⁸⁵ Basi, niambieni ni nani mwanamke huyu amegusa? Mimi niko umbali wa yadi ishirini na tano kutoka kwake. Yeye alimgusa Yesu Kristo, yule Kuhani Mkuu. Mnaamini hayo?

¹⁸⁶ Ninamtazama mwanamke niliyezungumza naye.

Mwanamke huyu, ninamtazama moja kwa moja, kwa sababu anaomba kwa bidii sasa kwa ajili ya mwanamume fulani. Yeye aliniambia alikuwa mwanamume. . . Hakuniambia cho chote juu yake, bali jina lake ni Bi. Waldrop. Yeye anatoka Phoenix. Alifufuliwa kutoka kwa wafu, na daktari wake akaja na X-ray na kuonyesha kansa moyoni mwake. Akafia kwenye mstari wa maombi. Imekuwa muda gani, Bi. Waldrop? Miaka kumi na minane iliyopita, naye yuko pale usiku huu, ushuhuda ulio hai.

¹⁸⁷ Madaktari wake wakaja mkutanoni, wakaleta. . . Kasema, “Mwanamke huyu anaweza kuishi vipi?” Bali ndiye huyu, na hamna hata dalili yake. Yeye alileta mtu fulani, naye anamwomba. Naam, anakufa sasa kwa ugojwa wa sukari.

Sasa, nilijua hilo. Bali kwa kuwa unaomba . . . Unajua simjui, Bi. Waldrop.

¹⁸⁸ Ametoka Missouri, na jina lake ni Bw. Cooper. Hiyo ni kweli. Sasa, unaamini? Unaweza kwenda nyumbani ukapone, Bwana. Ni juu yako kama utaamini hilo.

¹⁸⁹ Hapa kuna mwanamke, naye anaugua ugonjwa wa pumu, maradhi mabaya. Yeye hatoki hapa. Anaketi kule nje kwenye makutano, mbali kule. Natumai atapata . . . yeye si mwenyeji wa hapa; ametoka Georgia. Binti Mckenny, unaamini kwa moyo wako wote na kuamini ya kwamba Mungu atakuponya? Simama kwa miguu yako kama u mgeni kwangu na hiyo ni kweli. Yesu Kristo amekuponya. Unaamini?

¹⁹⁰ Nyuma yangu, kuna mwanamume anayeketi nyuma yangu. Anawasiliana na Mungu. Naye anachotaka, ana mtoto mchanga anayeugua moyo. Naye mtoto huyo ana mnog'ono moyoni mwake, ndivyo daktari alivyosema. Na jina la mtu huyo ni Bw. Cox. Simama, Bw. Cox. Yeye alimwambia Sara aliyokuwa akiwaza nyuma Yake.

¹⁹¹ Mle upande mwingine wa marefu ya kanisa, nyuma kidogo, kuna mtu asiye mwenyeji wa hapa, bali anatoka New Mexico. Sijapata kumwona kamwe maishani mwangu mwote. Ninamtazama sasa, yuko nyuma yangu. Ametoka New Mexico, naye mtu huyu ana msichana anayemsikitikia. Naye huyo msichana ana shida mdomoni. Ni . . . Kaa la kinywa chake ndilo baya. Mtu huyo jina lake ni Bw. West. Je, unaweza kusimama, Bwana? Mimi ni mgeni kabisa kwake, bali Bwana Mungu atamponya mtoto wake. Je, unaamini sasa kwa moyo wako wote?

¹⁹² Je, ni wangapi wenu wanamini sasa kwa mioyo yenu yote? Sasa, si Yesu Kristo ndiye yeye yule jana, leo, na hata milele? Je, mnamkubali sasa kama Mwokozi wenu, inueni mikono yenu. Je, mnamwamini kama mponyaji wenu?

¹⁹³ Hapa mna mtu anayeketi hapa kiwete ama cho chote kile, ameketi kitandani. (Waweza kunisikia kwa maikrofoni hii? Sikujui wewe; wewe ni mwanamke tu aliyelala pale. Ningaliweza kukuponya, ningekuponya. Siwezi kukuponya. Ni mtu tu . . .? mwanawe. Sikujui wewe. U mwanamke, mimi mwanamume. Hii ndiyo mara ya kwanza tunayokutana maishani, nakisia . . .? iliyokuleta. Bila shala hii ndiyo mara yako ya kwanza hapa . . .? Umetoka mbali sana. Umetiwa kivuli cha mauti. Una kansa . . .? . . . Madaktari hawawezi kukufanyia cho chote sasa. Ni kweli. Nawe huna budi kufa. Hao madaktari hawawezi kukufanyia cho chote.

¹⁹⁴ Siku moja kulikuweco watu watatu wenye ukoma langoni mwa Samaria. Nao wenye ukoma hao wakasema, "Mbona tuketi hapa hata tufe, maana watoto wote wanakufa kwa njaa nao wanakula watoto wao wenyewe kwa wenyewe." Wakasema "Kama tukishuka kwenye ile kambi ya adui, wale Washuru . . .

Kama watatuua, tutakufa haidhuru. Na kama watatuokoa, tutaishi.” Nao wakatamia nafasi hiyo. Na kwa imani hiyo, hawakujiokoa tu wenyewe bali kundi lote.

¹⁹⁵ Naam, utakufa, hauwezi ukaishi. Bali haujaulizwa kwenda kwenye kampi ya Gidioni, bali umekaribishwa kwenye nyumba ya Baba...?

¹⁹⁶ Unakufa kwa kansa; hauwezi kuishi nje ya Mungu. Wewe si mwenyeji wa mji huu; hautoki humu; umetoka mbali sana. Umetoka Milwaukee. Kweli...?...Naam. Unaamini? Je, utamkubali Mungu sasa kama mponya wako? Iwapo utafanya hivyo, haijalishi u mnyonge vipi, ulivyolemewa kitandani, naamini ningalikuwa mahali pako ningaliinuka katika jina la Yesu Kristo...?...kitanda chako na uende nyumbani ukaishi kwa utukufu wa Mungu. Unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu, basi inuka uende nyumbani, ukapone. Usiogope; ondoka kitandani. Mungu atakuponya. Ona?

¹⁹⁷ Mtu fulani amshikilie ili apate kusimama na kupata nguvu. Je, unamwamini Mungu? Mwache tu apate nguvu kidogo; atapona. Ndivyo hivyo dada. Ndiye huyu akiondoka katika Jina la Bwana Yesu.

¹⁹⁸ Hebu na tusimame na kumpa Mungu shukrani. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele...? Bwana Yesu Kristo awabriki. 

HUYU MELKIZEDEKI NI NANI? SWA65-0221E

(Who Is This Melchisedec?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Februari 21, 1965, kwenye Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2011 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org